

**MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WADAU WENGINE WA SHULE ZA
SEKONDARI KUHUSU SHENG: KIFANI CHA SHULE YA UPILI YA JAMHURI,
NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

NA

REUBEN W. BARASA

C50/80365/2015

**IDARA YA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

2018

Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa na kutahiniwa katika chuo kikuu chochote kingine.

Sahihi _____ Tarehe _____

Barasa W. Reuben (Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi tuliochaguliwa na chuo kikuu cha Nairobi

Sahihi _____ Tarehe _____

Dkt. Ayub Mukhwana (Msimamizi)

Sahihi _____ Tarehe _____

Prof. Iribe Mwangi (Msimamizi)

Tabaruku

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu (Jackson na Barta), ndugu yangu David, mke wangu Cecil na watoto wetu Stacie na Maya ambao waliweka ndoto yangu ya masomo hai. Uvumilivu wao, usaidizi wao wa kifedha na wa mawazo ni zawadi kubwa kutoka kwa Mungu ambayo walinipa katika kipindi hiki cha utafiti na masomo haya.

Shukrani

Shukrani zangu za dhata ziwaendee wasimamizi wangu Dr. Ayub Mukhwana na Prof. Iribe Mwangi kwa usaidizi na mwongozo wao wa kitaaluma katika kipindi chote cha utafiti huu. Usaidizi na ukosowaji wao muhimu ndio ambao umeikuza kazi hii kuwa jinsi ilivyo.

Shukrani zangu za dhata pia ziwaendee wahadhiri wangu, Prof. John Habwe, Dkt. Prisca Jerono, Leo Sanja, Prof. Rayya Timammy, Dkt. Zaja, Prof. Kineene Wa Mutiso, Prof. Mbathia Mwenda, Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Jefwa Mweri kwa mwongozo na masomo yao katika somo la isimu. Uongozi wao, kujitolea kwao na ufahamu wao wa isimu ndiko kuliko nitia moyo sana. Kila mmoja wenu alichangia pakubwa katika kazi hii. Shukrani zaidi kwake Dkt. Ayub Mukhwana kwa kunijaza kuhusu swala la Isimujamii ambalo nimelishughulikia kutokana na ujuzi wake wa mada hiyo.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu Ronald Aloo, Bernard Mulati, Maureen Wafula, Cyrus Moindi, Faith Ngila, Sr. Agnes Kwaka, Edward Mariga, Naomi Geke, Lydia Moraa, Irene Kilingo, Grace Mwet, John Mwaniki, Gloria Kirui, Fanuel Akollo, Edwin Otuoma. Ilikuwa fahari kupambana na kujishughulisha pamoja kwa miaka miwili katika kozi ya isimu. Mlikuwa kiungo muhimu kwa kunitia moyo kila mara.

Shukrani zangu za dhata zinawaendea wasaidizi wangu ambao ni wanafunzi na wadau wa Shule ya Upili ya Jamhuri waliotupa habari kuhusu lugha ya Sheng. Ufahamu mzuri kuhusu lugha ya Sheng ulikuwa wa manufaa sana katika utafiti huu. Nawashukuru wote kwa muda wenu katika kuchangia kupata habari kuhusiana na utafiti huu.

Shukrani kwa wazazi wangu (Jackson na Berta), kakangu David na mke wangu Cecil kwa usaidizi wao wa kifedha na kunitia moyo kila wakati. Kila mmoja alinihimiza kutia bidii zaidi. Walinifunza umuhimu wa uvumilivu na kufanya bidii. Nawakabidhi ufanisi huu.

Kwa jamii yangu kwa jumla, marafiki ambao walinitakia mema, kunihimiza na kunisaidia kila nilipohitaji usaidizi katika kipindi chote cha utafiti, asanteni sana.

Nawashukuru wote kwa kujitolea kwenu hadi kuifanya kazi hii kuwa ya kufana na kuweza kufaulu. Namwomba Mungu ambaye alinipa nguvu na hifadhi ambayo ilinisaidia kufanikisha kazi hii awabariki kila mmoja wenu.

Ikisiri

Tasnifu hii imetafiti mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine katika shule ya sekondari ya Jamhuri jijini Nairobi kuhusu lugha kipindi ya Sheng. Kazi hii imelenga hasa kubaini iwapowanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri wanaenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu, kutambua miktadha ambamolugha ya Sheng hutumiwa katika shughuli zao za kimawasiliano na pia, kutathmini mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu wa wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii na vile vile kutafiti mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri kuhusiana na matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Ili kutimiza malengo haya, utafiti huu umetumia nadharia ya kisaikolojia ya jamii ili kuweza kufanikasha malengo yetu. Sampuli iliyotumika kwa kupata data ya utafiti huu ilihusu jumuiya nzima ya shule ya upili ya Jamhuri jijini Nairobi. Uteuzi huu umefanywa kimaksudi. Mbinu zilizotumika katika kupata data ya kazi hii ilihusu matumizi ya hojaji na vile vile mahojiano mbali na kusoma katika maktaba hasaa kuhusu swala zima la Sheng na nadharia iliyotumika katika utafiti huu umebaini kuwa; wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri wanaenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu kutokana na mielekeo yao kuhusu Sheng, miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri hutumia lugha ya Sheng katika shughuli zao za kimawasiliano imedhihirikakuwa ni shuleni, nyumbani, sehemu za burudani na hata sokoni, mitazamo na mielekeo nayo ya wazazi na walimu wa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii ilikuwa chanya kutokana na mielekeo yao na pia mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusiana na matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi ulikuwa mkubwa kutokana na mielekeo yao chanya kuhusiana na lugha ya Sheng. Sababu kuu ya kuchangamkia Sheng ni kuwa inatumiwa na vijana na wazee vijana wa jinsia zote kufumbia mambo na kwa hiyo kuifanya kuwa lugha ya kundi ndani.

YALIYOMO

Ungamo	i
Tabaruku.....	ii
Shukrani	iii
Inkisiri	iv
Yaliyomo	v
Maelezo ya dhana	ix

SURA YA KWANZA

USULI WA MADA

1.1 Utangulizi.....	01
1.2 Usuli wa mada.....	01
1.3 Tatizo la utafiti.....	02
1.4 Maswali ya utafiti.....	02
1.5 Malengo ya utafiti	02
1.6 Umuhimu wa utafiti.....	03
1.7 Upeo na mipaka ya utafiti.....	03
1.8 Yaliyoandikwa	04
1.8.1. Yaliyoandikwa kuhusu lugha ya vipindi	06
1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Sheng.....	08
1.8.3 Yaliyoandikwa kuhusu athari ya lugha ya Sheng.....	09

1.8.4. Swala la Sheng na mielekeo katika kazi nyingine.....	10
1.9 Nadharia	13
1.10 Haipotesia	14
1.11 Mbinu za utafiti.....	14
1.11.1 Uteuzi na maelezo kuhusu mahali pa kufanyia utafiti.....	14
1.11.2 Idadi ya hadhira ya kufanyiwa utafiti.....	15
1.11.3 Mchakato wa kuteua sampuli.....	15
1.11.4 Asili ya data.....	16
1.11.5 Ukusanyaji wa data na vifaa vitakavyotumiwa.....	16
1.11.6 Maswala ya kimaadili.....	16
1.11.7 Uchanganuzi wa data.....	17

SURA YA PILI

MIELEKEO KATIKA SERA YA LUGHA KENYA KUFIKIA SASA

2.1 Utangulizi	18
2.2 Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya kihistoria	18
2.2.1 Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya enzi ya ukoloni.....	19
2.2.2 Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya baada ya ukoloni.....	24
2.3 Katiba ya Kenya 2010.....	30
2.3.1 Sera ya lugha nchini Kenya kwa mujibu wa katiba ya Kenya 2010.....	31
2.4 Hitimisho	32

SURA YA TATU

MATOKEO YA UTAFITI

3.1	
Utangulizi.....	34
3.2 Mielekeo ya wanafunzi na wadau kuhusu Sheng.....	34
3.2.1 Wanafunzi	34
3.2.2 Walimu	39
3.2.3 Wafanyikazi wasio walimu	41
3.2.4 Wazazi	44
3.3 Hitimisho	47

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA MJADALA KUHUSU MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi.....	49
4.2 Uchanganuzi wa matokeo ya utafiti	49
4.2.1 Kubaini iwapo wanafunzi na wadau wengine wanaenzi lugha ya Sheng	49
4.2.2 Miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia Sheng.....	52
4.2.3 Mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya Sheng nawanafunzi	54
4.2.4 Mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu Matumizi ya Sheng miongoni mwa wanafunzi	56
4.3 Hitimisho.....	58

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITAJI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi	60
5.2 Muhtasari	60
5.3 Mahitimisho	61
5.4 Mapendekezo.....	62

MAREJELEO.....	64
-----------------------	-----------

Kiambatisho 1 (Hojaji za wanafunzi)	ix
--	-----------

Kiambatisho 2 (Hojaji za walimu)	xiv
--	------------

Kiambatisho 3 (Hojaji za wafanyikazi wasio walimu)	xix
---	------------

Kiambatisho 4 (Hojaji za wazazi)	xxiv
---	-------------

Maelezo ya dhana zilizotumiwa

Katika utafiti huu kuna baadhi ya dhana ambazo zimetumika mahususi kwa ajili ya utafiti huu. Dhana zenyewe ni kama ifuatavyo:

Lugha ya kwanza - lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza kabisa kabla ya lugha nyingine yoyote. Lugha hii si lazima iwe lugha ya mama ya mtu husika. Katika muktadha ya taifa la Kenya lugha hii inaweza kuwa lugha ya mama, Kiingereza, Kiswahili, lugha kipindi ya Sheng au hata lugha ya ishara ya Kenya.

Lugha ya pili - lugha ambayo mtu hujifunza baada ya lugha ya kwanza. Katika taifa la Kenya, mfumo wa elimu pamoja na hali ya wingilugha huwafanya wakenya wawe na lugha nyingine baada ya ile ya kwanza. Lugha hii ya pili yaweza kuwa; Kiswahili, Kiingereza, lugha kipindi ya Sheng au lugha ya moja wa wazazi.

Wingilugha - ni hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika shughuli za mawasiliano. Hali hii ya wingilugha inaweza kuwa inayohusu ujuzi wa lugha mbili au zaidi kimaandishi, kiusomaji au kiusemaji.

Utatulugha - ni hali ya kuwa na uwezo wa kuzungumza na kuelewa lugha tatu kwa ufanisi. Hayta hivyo yafaa kukumbukwa kwamba ile lugha inayotajwa mwanzo na mwana utatulugha ndiyo inayopendelewa katika wazo zima la utatulugha. Kwa hivyo, vipo viwango tofautitofauti vya utatu lugha kutegemea malengo na manufaa yanayotokana na hali hii ya utatulugha.

Msimbo - namna ambavyo kundi fulani la watu huwasiliana kwa kutumia miundo fulani ya maneno, nambari na ishara zinazowakilisha ujumbe fulani. Kwa hali hii kila lugha hujitokeza kama msimbo. Hata hivyo, msimbo unaofafanua mambo kiwaziwazi hujulikana kama msimbo pana. Huku unaotoa vidokezo tu na kufahamika na kundi ndani hujulikana kama msimbo finyu. Kama alivyosema (Barne Steer - 1972)

Tasfida - ni matumizi ya lugha ya heshima au lugha inayopunguza makali. Lugha hii hutumia maneno yanayojulikana kama maneno mwiko na

husema kitu kana kwamba sicho. Hali hii hujulikana vile vile kama kuvalisha lugha nguo.

Uchanganuzi makosa-mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi.

Mielekeo - ni mahali ambako fikra za mtu zinakoelekezwa hasaa kuhusu jambo fulani.

Wazee vijana - ni wazee au watu wa rika la makamo ambao watasikika wakitumia lugha ya Sheng na ambayo huambatishwa hasa na vijana nchini Kenya. Hawa wanaitwa wazee vijana kwa sababu wamekaidi mipaka ya umri wao.

SURA YA KWANZA

USULI WA MADA

1.1. Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo ya kimsingi kuhusu utafiti huu kama vile; usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na pia mbinu za utafiti.

1.2. Usuli wa mada

Lugha ya Sheng inazungumzwa kwa wingi jijini Nairobi na katika miji mingine ya nchini Kenya (Abdulaziz na Osinde 1997, Osinde 1986, Mukhwana 2008). Utafiti huu umeangazia shule ya upili ya Jamhuri iliyomo jijini Nairobi na ipatikanayo mitaa ya Mashariki kulikoanzia lugha ya Sheng (Osinde 1986). Katika taifa la Kenya ambapo shule zimegawika kutatu (shule za kitaifa, shule za mkoa na shule za majimbo madogo) Jamhuri kama shule ya mkoa itaunganisha shule zote Kenya na kutoa picha halisi katika muktadha huu kuhusu mielekeo dhidi ya Sheng. Nairobi ni mji mkuu wa Kenya na kwa hiyo, mambo yanayopitikia jiji hili yanakuwa ni kiwakilishi cha Kenya nzima. Kwa hali hii, mielekeo kuhusu lugha ya Sheng katika shule ya Jamhuri ipatikanayo Nairobi inaweza kuchukuliwa kuwa ni picha kamili na halisi kuhusu Kenya nzima kwa jumla.

Kwa kuwa lugha hii ya Sheng pia inakisiwa kuanzia au kukua kutoka katika vitongoji duni Kenya hasaa jijini Nairobi, shule ya upili ya Jamhuri ilikuwa mwafaka katika kufanya utafiti huu kwa kuwa ipo karibu na vitongoji hivi na pia wanafunzi wengi wanaosomea shuleni hapo wanatoka katika vitongoji hivi.

Kwa mujibu wa ayasemayo Mukhwana (2014), mielekeo huwa na nafasi kubwa sana katika kujifunza au kujua lugha hasa katika sehemu ambapo kuna matumizi au wazungumzaji wa wingilugha. Kulingana naye, anasema kuwa mielekeo ya wazungumzaji wa lugha huathiriwa pakubwa na sehemu ambamo wazungumzaji hao wamo na pia lugha yao ya kwanza. Ogechi (2002) na Shitemi (2001) wanaelezea kuwa Sheng ni msimbo wa kijamii unaotumiwa hasa mijini na mashambani nchini Kenya. Maoni haya yamefungamanisha Shengna kundi la vijana ingawa hata watoto na wazee pia hutumia lugha hii ya Sheng katika mazungumzo yao ya kila siku hasaa katika muktadha wa nyumbani.

Utafiti kuhusu mielekeo walio nayo wanafunzi wa shule za upili kama huu tunaoufanya ni muhimu kwa kuwa unatoa picha halisi kuhusu mustakabali wa lugha hii ambao vile vile ni muhimu kwa wapangaji wa lugha na kwa sera ya lugha nchini.

1.3. Tatizo la utafiti

Mielekeo kuhusu jambo lolote lile maishani yaweza kuwa ama chanya au hasi. Utafiti huu unachunguza mielekeo walionayo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu lugha pendwa ya Sheng. Kwa kuwa lugha hii iko nasi, inastahili kutafitiwa na ukweli kuhusu kubainishwa (Kachipela, 2014; Babusa, 2005). Tumekuwa na lalama kuwa lugha hii inahasiri matokeo ya somo la Kiswahili katika mitihani ya kitaifa. Wakati huo huo, katiba ya taifa la Kenya (2010) inawapa wakenya uhuru wa kujitambulisha na kuchangamkia lugha na utamaduni wao uhiari. Kutokana na hali hii maswali kadhaa yanaibuka. Je, lugha kipindi ya Sheng ina nafasi gani katika fikra za vijana wa walio wengi nchini Kenya? Je, nafasi ya mielekeo niipi katika mustakabali wa lugha msimu ya Sheng hasaa ikikumbukwa kuwa ulimwenguni lugha msimu zimekuja kuchangia lugha msingi msamiati wake na muundo wake wa jumla? Haya ni baadhi ya maswali ambayo utafiti huu unanua kuyajibu kutokana na uchunguzi wa mielekeo ya wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri jijini Nairobi kuhusiana na lugha ya Sheng.

1.4. Maswali ya utafiti

Kutokana na malengo ambayo tumeyaorodhesha, utafiti huu una maswali ya utafiti yafuatayo;

- i. Je, wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri huenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu?
- ii. Je, ni mikitadha ipi ya mawasiliano ambayo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano?
- iii. Je, mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu wa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii ni ipi?
- iv. Je, wafanyikazi wasio walimu huchangia vipi matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri?

1.5. Malengo ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo;

- i. Kubaini iwapo wanafunzina wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri wanaenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu.
- ii. Kutambua miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri hutumia lugha ya Sheng katika shughuli zao za kimawasiliano.
- iii. Kutathmini mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu wa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii.
- iv. Kutafiti mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri kuhusiana na matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

1.6. Umuhimu wa utafiti

Ni ukweli dhahiri kuwa vijana ndio wengi ulimwenguni hapa. Kile walichokishikilia vijana hakiwezi kupuuzwa kwa vyovyote vile. Hii ndiyo sababu kuu ya kutafiti mielekeo ya vijana kuhusiana na lugha vipindi ya Sheng. Mielekeo yao kuhusu lugha hii itawasaidia wapangaji lugha na wanasera ya lugha nchini Kenya kuweza kuipa lugha hii nafasi yake katika hali ya wingilugha ipatikanayo nchini Kenya. Isitoshe, vijana tunaowatafiti ndio watakao kuwa viongozi wa kesho. Kwa hali hii mielekeo yao kuhusu lugha ya Sheng itahisika siku za baadaye nchini hapa na kwa hiyo haipaswi kupuuzwa.

1.7. Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu unajaribu kujibu maswali kuhusiana na mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari kuhusiana na Sheng.

Tumeweza kuwashirikisha wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri ambayo imo katikati mwa jiji kuu la Nairobi kunako aminika kuwa kitovu cha lugha hii ya Sheng. Pia shule ya upili ya Jamhuri kwa kuwa ni ya mkoa/jimbo, imeweza kuwakilisha na kutoa picha kuhusu shule zote nchini Kenya. Wanafunzi, walimu, wazazi pamoja nawafanyikazi wengine wasio walimu wameweza kusaidia katika kujibu hojaji na pia katika mahojiano ya moja kwa moja.

Hata hivyo, hatujaweza kuzuru na kupata maoni ya watu wengine ambao sio wazazi au wafanyikazi wasio walimu katika mitaa ambamo lugha Sheng inatumiwa sana na pia wanakozaliwa wanafunzi hawa wanaozungumza lugha ya Sheng. Chaguo la kutumia shule ya upili ya Jamhuri pia imetumiwa kama kiwakilishi cha wazawa kutoka mitaa hiyo na pia shule zote za sekondari nchini Kenya na hivyo basi hatujaweza kuzuru shule zingine.

Pia maswala kama vile athari ya lugha ya Sheng katika kujifunza Kiswahili sanifu shuleni na katika mawasiliano na shughuli za kila siku hayajaweza kugusiwa.

1.8.Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kuna wataalamu wengi ambao wamefanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha vipindi na athari zao kwa lugha zingine. Hata hivyo nia yetu ya kuchunguza mielekeo ya wanafunzi kuhusu Sheng katika shule za sekondari Nairobi ni kuwa kati ya kazi hizi zote zilizoandikwa, hakuna ile iliyozungumzia mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari kuhusiana na Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, Nairobi. Hata hivyo tumeyatilia maanani yote yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti.

Abdulaziz na Osinde (1997) wameelezea asili na chimbuko ya Sheng. Wameibuka na nadharia tete kuwa Sheng iliibuka katika mitaa ya Mashariki jijini Nairobi miaka ya sabini. Waandishi hawa wanaongezea kuwa kutokana na kupatikana kwa uhuru mwaka wa 1963, idadi ya wakazi wa Nairobi iliongezeka kwa kasi kutokana na kuhama kwa watu kutoka sehemu za mashambani hadi mjini kwa lengo la kutafuta kazi sehemu za viwandani. Ingawa watu hawa walilazimikakutumialugha ya Kiswahili katika shughuli zao za mawasiliano, walikichukia kwa sababu kilidunishwa na sera za lugha za kikoloni. Watoto wa wafanyikazi hawa walilazimika kuishi katika jamii ya utatulugha, yaani lugha ya Kienyeji, Kiswahili na Kiingereza. Ili kuepuka matatizo ya kimawasiliano, vijana hao walibuni namna ya mawasiliano iliyofuata sarufi ya Kiswahili. Namna hii ya mawasiliano ndiyo ilitokea na kuwa Sheng baadaye. Hata hivyo, Mazrui (1995) na Mpande (1990) wanasema kuwa Sheng ilianza mnamo miaka ya thelathini.

Mukhebi (1986) anasema kuwa Sheng ni tukio lakitamaduni ambalo linafungamana sana na mawazo au fikra, hisia na matakwa ya watumiaji wake. Osinde (1986), Abdulaziz na Osinde (1997), Mazrui (1995) na Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanakubaliana na maoni haya na kuongezea kuwa Sheng ni lugha kipindi ya lugha ya Kiswahili inayohusishwa sana na vijana. Maoni haya ya waandishi hawa tunakubaliana nayo kuwa Sheng ni lugha kipindi kwani ni lugha iliyo na msamiati uliojikita katika msimu fulani na hutoweka pindi tu msimu huo unapotamatika. Vile vile lugha kipindi huwa na mbinu za kiusemi zinazowatambulisha na kuwaunganisha wazungumzaji wake. Sheng imeungama sifa hizi kwani huwa na msamiati unaobadilikabadilika jinsi wakati unavyosonga na pia huwaunganisha wazungumzaji na kuwafanya kujihisi ni wa kundi moja. Lave na Wenger (1991) wanaeleza kuwa Sheng ni lugha kipindi ya Kiswahili inayotumiwa hasa na makundi mahususi ya vijana

nchini Kenya. Makundi haya huwakilisha hali ya upanuzi wa msamiati na utamaduni wa Kenya.

Mkangi (1984) naye anasema kuwa Sheng ni lugha mseto au lugha 'kiunzi' ya kizazi kipya cha vijana wa mijini na hata mashambani nchini Kenya. Anaongezea kuwa muundo wa kisarufi wa Sheng hufanana na wa Kiswahili na lugha nyinginezo za kibantu ila Sheng hutumia maneno mengi mapya ya kubuniwa na ya kukopa kutoka lugha zingine mbalimbali kama vile Kiingereza, Kikikuyu na Kijaluo.

Webb na Kembo-Sure (1992) wanasema kuwa wingilugha nchini Kenya kulisababisha kuzuka kwa lugha zingine kama Sheng.

Spypoulos (1987) anaeleza kuwa, Sheng ilianza miaka ya hamsini na kutia fora miaka ya sabini. Sababu kuu ya madai haya ni kuwa, majarida na magazeti yaliyokuwa na Sheng yalitokea katika miaka hiyo ya sabini.

Gathiora (2002) anasema kuwa, Sheng ilizuka kutoka maeneo tofauti ya makazi katika mitaa ya Mashariki mwa jiji kuu la Nairobi kama vile Kaloleni na Bahati. Sheng imeenea kila mahali, lakini sana jijini Nairobi katika mitaa kama vile Kangemi, Kawangware na hata Githurai.

Kobia (2006) anasema kuwa, katika miaka ya sabini, wazungumzaji wa Sheng waliunda baadhi ya maneno kutoka nyuma kuelekea mbele badala ya kuzingatia kanuni za kawaida za kuunda maneno. Mbinu hii ya uundaji wa maneno ya Sheng imetumika hadi sasa. Kwa mfano; risto (stori), lembe (mbele), shoke (kesho) na pia daso (soda). Mifano hii inaonyesha kuwa silabi za neno hupanguliwa na kupangiliwa upya na huku zikipewa muundo wa kinyumenyume. Kulingana na mwandishi huyu, haya yote yalifanywa kwa lengo la kuwasiliana kwa lugha ambayo watu wengi hawangeweza kuifahamu.

Mbaabu na Nzunga (2003) nao wanaongezea kuwa, kufikia miaka ya sabini Sheng ilikuwa imeenea sio tu Nairobi bali pia miji mingine nchini. Madai ya waandishi hawa wote kuhusu asili na chimbuko la Sheng yanatofautiana na ndiyo sababu inayompelekea mwandishi mwingine; Ngesa (2012) kusema kuwa hakuna asili moja ya Sheng.

Licha ya tofauti za maoni ya wataalamu hawa, wengi wanaonekana kukubaliana kuwa Sheng ilizuka katikati ya miaka ya sitini na sabini katika sehemu za Mashariki mwa jiji kuu

la Nairobi kama vile Mathare, Kaloleni, Dandora, Kayole na mitaa mingine mingi iliyoko Mashariki mwa jiji. Kwa kuwa wanafunzi wengi katika shule ya upili Jamhuri wamezaliwa, kulelewa na hata bado wanaishi katika mitaa hii, walituwezesha kupata na kujua mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule za sekondari Nairobi kuhusiana na lugha ya Sheng.

Sehemu ambamo wazungumzaji wamo husababisha kuwepo na upendeleo wa lugha fulani, kwa mfano katika mji wa Nairobi, wazungumzaji wengi wa lugha ya Sheng hupatikana katika vitongoji duni kama vile Mathare, Kibera na vingine vingi. Utapata kuwa, sehemu hizi kutokana na kusongamana kwa watu, wazungumzaji hawa hutafuta lugha mbadala ili kuweza kuficha maana ya mazungumzo yao kutoka kwa kundi lingine. Vilevile, katika maeneo haya, utapata kuwa watu wanaoishi hapa ni wanaozungumza lugha ya mama tofauti tofauti na hivyo basi wanatafuta njia yakuweza kuwasiliana kwa lugha ambayo kila mmoja anaifahamu na kuielewa.

Lugha ya kwanza ya wazungumzaji pia huathiri mielekeo ya wazungumzaji hawa katika kuzungumza lugha ya Sheng. Hii mara kwa mara hutokana na kutangamana kwa wanafunzi ambao wanazungumza lugha tofauti tofauti za kwanza na hivyo basi kutaka kutumia lugha moja ambayo itawawezesha kuwasiliana. Hata hivyo, kuna lugha zingine kama vile Kiingereza na Kiswahili ambazo zaweza kutumiwa kwa kuwasiliana miongoni mwa wanafunzi hawa bali wao huegemea kutaka kutumia lugha ya Sheng zaidi kwa sababu mbalimbali. Tulipofanya mahojiana na baadhi yao wakati wa utafiti huu, tulipata kujua kuwa wanafunzi wengi huipendelea Sheng kwa kuwa ni rahisi kutokana na msamiati ambao hutungwa na wazungumzaji wenyewe, haizingatii kanuni zozote za kiasarufi. Pia lugha ya Sheng huweza kuficha maana na ndio maana wazungumzaji wengi huipenda kutumia kwa nia ya kuficha maana kutoka kwa kundi fulani la watu. Hii ndiyo iliyotusababisha kufanya utafiti huu ili kujua mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari kuhusiana na lugha ya Sheng.

1.8.1. Yaliyoandikwa kuhusu lugha ya vipindi

Lugha ya vipindi ni lugha ambayo ina maneno ya misemo iliyojikita katika kipindi fulani cha wakati na hutoweka pindi tu kipindi hiki kinapoisha. Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaongezea kuwa lugha vipindi huwa na mbinu za kiusemi zinazowatambulisha wazungumzaji wake. Naunga mkono maoni ya wataalamu hawa kwani lugha vipindi nyingi huwa na visawe vingi na vingine huachwa kutumiwa na vingine vipya kubuniwa jinsi wakati unavyosonga.

Gathiora (2002) anasema kuwa lugha kipindi ya Swanglish huzungumzwa nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili ikiwa ndiyo lugha rasmi nchini humo. Swanglish ni lugha kipindi ya lugha ya Kiswahili inayohusisha lugha za kienyeji, Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Vijana wengi hutumia lugha hii sana katika muziki na hata miundo mpya ya kimavazi. Githiora ameendelea kusema kuwa Swanglish imeanza kutumiwa na vijana hata katika muktadha wa darasani kwa hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili. Mifano ya Swanglish ni kama vile; mzuka (vizuri zaidi) na bomba (sawasawa). Kupitia mifano hii ni dhahiri kuwa maneno hupewa maana tofauti ili kuakisi mfumo wa lugha kipindi hiki. Kama neno 'bomba' katika Kiswahili sanifu lina maana ya kifaa chenye shimo katikati cha kupitishia maji safi au taka na hata pia moshi ilhali neno hili limepewa maana tofauti katika Swanglish kwa maana ya sawasawa.

Nguemo (2008) ameangazia lugha kipindi ya Naijalingo nchini Nigeria ambayo ni lugha kipindi ya Kiingereza. Lugha ya Kiingereza ndiyo lugha rasmi nchini Nigeria. Naijalingo hupata maneno yake kutoka kwa lugha za Yoruba, Igbo, Hausa na Kiingereza. Naijalingo hutumiwa sana na vijana kwa lengo la kufanikisha mawasiliano yao na kubana ujumbe kutoka kwa wale wasiohusika. Lugha kipindi hii huleta utata wa maana hasa inapotumika katika muktadha wa darasani. Hii ni kwa sababu maneno yenye asili ya Kiingereza hupoteza maana zao za asili kila yanapotumika katika Naijalingo. Msamiati wa Naijalingo pia hujitokeza katika kazi zilizoandikwa na wanafunzi na hivyo kuleta utata wa kimaana. Mifano ya Naijalingo ni kama; 'how body' (habari yako). Katika mfano huu, maneno ya Kiingereza yametumiwa kwa maana tofauti na maana asili.

Amanda (2011) ameangazia lugha kipindi ya Namlish nchini Namibia ambapo Kiingereza ndio lugha yao rasmi. Namlish ni lugha kipindi ya Kiingereza nchini Namibia. Namlish hutumiwa sana na vijana hawa katika mawasiliano yao. Hata hivyo Namlish huathiri sana utendaji wa vijana hawa hasa kila wakati wanapotumia lugha ya Kiingereza. Namlish hupata maneno yake kutoka kwa lugha ya Karongo, Darama, Oshiwambo na pia Herero. Mifano ya Namlish ni kama; washup? 'nini cha mno' ambalo likizingatiwa kwa Kiingereza sanifu lafaa kuwa *what's up?*. Hivyo basi ni dhahiri kuwa Kiingereza kinachotumika katika Namlish si sanifu.

Branford (1980) ameangazia lugha vipindi za Afrikaanerism nchini Afrika Kusini. Lugha ya Kiingereza nimoja wapo ya lugha rasmi nchini Afrika Kusini. Afrikaanerism ni lugha ya vipindi za lugha za Kiingereza Afrika Kusini. Lugha vipindi hizi huhusisha lugha ya Afrikaans, Kiingereza na lugha zingine za kienyeji. Wazungumzaji wa Afrikaans ni wenyeji

wa Afrika kusini wanaotumia lugha hii kama lugha ya kwanza na Kiingereza kutumiwa kama lugha ya pili. Mifano ya Afrikaanism ni kama vile; antie (mwanamke mwenye mamlaka fulani) na anties (maziwa ya mwanamke). Tofauti inadhihirika wazi kati ya Afrikaanism na Kiingereza.

Sabiti (2015) ameanzia lugha kipindi Uglishi inayotumika nchini Uganda. Nchini Uganda, lugha Kiingereza ndiyo lugha rasmi inayotumiwa katika shughuli zao mbalimbali za kila siku. Uglish hupata maneno yake kutoka lugha za Luganda, Kiingereza na lahaja zingine zinazotumika nchini Uganda. Kuzuka na kusambaa kwa Uglish kunasusha kiwango cha elimu nchini Uganda kwani mielekeo ya wazungumzaji wengi wanakitumia ilhali kwa upande wa masomo, ni lugha ya Kiingereza inayotumiwa. Mifano ya maneno ya Uglish ni kama vile; cowardice (woga), dirten (chafua). Kwa kuzingatia mifano hii miwili, tunaona kuwa lugha ya Kiingereza inayotumiwa katika Uglish si sanifu unapopata maana inayokusudia kutoa katika lugha ya Kiswahili. Ingawa mwandishi alijaribu kuonyesha namna Uglish inavyoathiri elimu nchini Uganda, maoni haya pia yatasaidia kupata mielekeo ya wazungumzaji hawa wa Uglish humo nchini.

1.8.2. Yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Sheng

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaeleza kuwa Sheng ina msamiati mpanuzi kutokana na kubadilikabadilika kwake. Maneno kama dem, manzi, mrembo na chic hutumiwa kwa maana moja ya kumaanisha au kurejelea msichana. Wanaendelea kusema kuwa Sheng ina wingi wa tasfida. Ni kweli kwani maneno kama; juala (kondomu), ukedi (ukimwi) na pia kuro (kahaba) huweza kusemwa bila uoga kwani yaficha makali ya meneno haya iwapo yangetamkwa kwa lugha ya Kiswahili sanifu.

Ndiku, Mwita na Ocharo (2014) wanayaunga maoni ya Muaka (2011) mkono kuwa wanajamii wana mielekeo tofauti kuhusu Sheng. Watu wanaoitumia Sheng wana mielekeo chanya kuhusu matumizi yake hivyo wanatetea matumizi yake. Maelezo haya ni muhimu sana na mwafaka katika utafiti huu kwani tunaangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa lugha ya Sheng katika shule za sekondari nchini Kenya; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, Nairobi.

Buliba na wenzake (2006) wanasema kuwa Sheng ilitokana na miingiliano baina ya vijana wa makabila mbalimbali walio ishi katika sehemu kama vile Huruma, Mathare, Kibera na Kaloleni. Kulingana na wao, muundo wa Sheng na wa Kiswahili hufanana. Maoni yao yalitusaidia kujua mielekeo ya wazungumzaji hawa kwani wanafunzi wengi katika shule ya

upili ya Jamhuri huishi katika sehemu hii na hivyo basi ikawa mwafaka kuweza kufanyia utafiti huu katika shule hiyo ya Jamhuri.

Mazrui (1995) anasema kuwa Sheng ni lugha kipindi inayohusishwa na vijana wanaotoka katika jamii yenye uwezo mdogo wa kiuchumi na wasio nao. Kazi hii ilitufaa kwa kuelewa asili ya Sheng hasa mada yetu ikiwa ni kujua mielekeo ya wazungumzaji wa Sheng kutokana na sehemu wanakoishi.

Mahu (2009) ameweza kuihusisha Sheng na makundi yenye kutenda mambo ambayo ni kinyume na maadili ya kijamii wanaoshiriki vitendo viovu kama vile; wanyang'anyaji, walanguzi wa madawa ya kulevya na pia wabakaji. Hata hivyo madai haya ni potovu kwani Sheng ina wingi wa tasfida ambazo zimeelezwa na wataalamu wengine waliotoa ufafanuzi kuhusu Sheng. Kazi hii hata hivyo ilikuwa muhimu kwani iliweza kutusaidia kujua na kuelewa mitazamo na mielekeo ya wanajamii kuhusu Sheng.

Njoroge (2014) ameelezea majukumu mbalimbali ya Sheng mjini Nakuru. Anadhihirisha kuwa Sheng ina majukumu mbalimbali na imepewa hadhi fulani mjini humo. Majukumu haya ni kama vile; kuwasilisha maudhui muhimu katika jamiikupitia muziki. Kama tunavyoangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu lugha hii ya Sheng na kuzingatia kuwa Nairobi pia ni mji, kazi hii itatufaa kwa kujua na kuelewa matumizi ya Sheng katika jamii.

Ogechi (2004) ameangazia jinsi leksemu za sheng huundwa na maana zilizojitokeza kutokana na leksemu hizi. Ingawa mwandishi huyu aliangazia namna ya kuunda leksemu za Sheng, sisi tumeangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu lugha ya Sheng na hivyo basi maoni yake hayatatufaa sana lakini ni muhimu kwa kusoma na kupata maoni yake yatakayofaidi kwa kuelewa kwa ziada.

Githinji (2006) anatoa maoni yake kuwa, tofauti za kileksia kati ya wazungumzaji wa Sheng hubainisha makundi madogo madogo ya wazungumzaji hawa. Ingawa kazi yake haitatufaidi sana, ni muhimu kuelewa makundi haya ya wazungumzaji wa lugha ya Sheng ili kuweza kujua mielekeo yao kuhusiana na lugha hiyo ya Sheng.

1.8.3. Yaliyoandikwa kuhusu athari ya lugha ya Sheng

Odhiambo (2013) ameangazia utata unaozuka kati ya waumini walio na umri wa juu na watoto wadogo wasioelewa Sheng katika dini za kisasa. Anaelezea kuwa waumini hawa huachwa nje hasa katika nyimbo za injili zinazoimbwa kwa lugha ya Sheng. Hii imekuwa

naumuhimu mkubwa katika kazi hii kwani tumeweza kuoanisha maoni na mielekeo ya wanajamii kuhusu athari za Sheng katika dini na elimu. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani kwani ameangazia athari ya Sheng katika dini ya Kikristo ilhali sisi tunaangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau katika shule ya upili ya Jamhuri, Nairobi kuhusu lugha ya Sheng.

Kachipela (2014) ameangazia makosa mbalimbali wanafunzi wa shule za msingi hufanya katika kazi zao za Kiswahili kutokana na lugha ya Sheng ambayo husababisha matokeo duni katika mitihani yao ya somo la Kiswahili. Utafiti wake unaonyesha kuwa Sheng huathiri utendaji wa wanafunzi katika kazi zilizoandikwa za Kiswahili. Utafiti wake ingawa ni tofauti na wetu ambao umeangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusiana na lugha ya Sheng. Ni muhimu katika kazi hii kwani unatoa wazi athari za lugha hii ya Sheng na pia kuwacha pengo la mielekeo ya wazungumzaji hawa ambalo tuliangazia ili kulijaza.

Okoto (2015) anasema kuwa, Sheng huwafanya watu waache kutumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhani ni ya Sheng. Kwa mfano neno ‘kuro’ katika Kiswahili ni mnyama wa porini anayefanana na kalungu lakini katika lugha ya Sheng, kuro lina maana ya kahaba. Pia neno kama ‘demu’ katika Kiswahili ni kitambaa kinachotumika kufungia maziwa ya mwanamke anapolima lakini katika lugha ya Sheng, demu lina maana ya msichana. Hivyo basi, hali hii inaashiria kuwa Sheng hupotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na utafiti wetu kwani yeye anaangazia athari ya lugha ya Sheng kwa lugha ya Kiswahili ilhali sisitunaangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusiana na lugha ya Sheng.

1.8.4. Swala la Sheng na mielekeo katika kazi nyingine

Lugha ya Sheng imeweza kuzungumziwa na waandishi wengi kama vile Abdulaziz, M. H. Pia maswala ya mielekeo ya wazungumzaji lugha husika pia imeweza kuangaziwa na waandishi kama vile Mukhwana A. (2008), katika makala yake “*Language Attitude in Urban Kenya*” ambapo ameangazia mielekeo ya wazungumzaji wa lugha mbalimbali kuhusiana na lugha yao ya kwanza.

Tafiti zingine mbalimbali zimefanywa kuhusu mielekeo, lakini nyingi zimejikita katika mielekeo ya wanafunzi kuhusu masomo, walimu au wanafunzi wengine. Gardner na Lambert (1972), Gardner (1985) na Baker (1992), ni miongoni mwa wataalamu waliotafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa lugha shuleni. Kwa mujibu wa Gardner

(1985), upataji lugha ya pili hutokea katika muktadha maalum wa kitamaduni na imani ya kijamii kuhusu umuhimu wa kujifunza lugha husika. Umuhimu wa lugha aliyojifunza mwanajamii huendelezwa katika uteuzi wa lugha na matumizi ya lugha husika baada ya kuifahamu. Hivyo basi kuna uhusiano kati ya sifa za kimielekeo na motisha na matumizi ya lugha (Gardner, ibid:174).

Hata hivyo, thamani na majukumu yanayotolewa kutekelezwa na lugha fulani huathiri mielekeo ya watu kuhusu lugha hiyo. Vilevile, mielekeo hiyo huathiri tabia za wanajamii katika kujifunza na kuitumia lugha husika (Mohochi, 2011). Utafiti wa Mohochi ulichunguza mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi kuhusu lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unatufaidi katika kutanabahi kuwa kutokana na mielekeo yao na ushawishi wao, wasomi kama vile walimu huathiri mielekeo ya wanajamii kuhusu majukumu na matumizi ya lugha husika. Kutokana na utafiti wa mtaalamu huyu, wanajamii hukuzwa katika kuwa na mielekeo hasi au chanya kuhusu lugha tofautitofauti kutoka walipokuwa wanafunzi hadi wanapokufika utu uzima na kupata nafasi za kazi ambapo wengine wao huwa walimu. Mielekeo yao kuhusu lugha itajidhihirisha hata wanaposhikilia majukumu yao ya kikazi.

Utafiti wa Lambert et al (1960) ulichunguza mielekeo ya wasikilizaji ambao walikuwa wazungumzaji wa Kiingereza na Kifaransa kuhusu lugha hizo mbili jijini Montreal (Canada). Wataalamu hawa walipata kuwa wasikilizaji wa lugha zote mbili waliipa lugha ya Kiingereza hadhi ya juu kuliko ile ya Kifaransa. Mwitikio huu wao ulitokana na sababu za kihistoria ambapo Kiingereza kilithaminiwa na wengi kama lugha ya kupata ufanisi wa kiuchumi na kijamii kuliko lugha nyingine yoyote ile. Kasumba hii imeendelezwa nchini Kenya ambapo, kutoka enzi ya ukoloni, Kiingereza pekee ndicho kilipewa jukumu la lugha rasmi hadi mwaka wa 2010 ambapo Kiswahili kilikwezwa kihadhi na kuwa lugha rasmi ya pili. Athari hii ya kihistoria ni mojawapo ya masuala yaliyotusukuma kufanya utafiti wetu, tukichunguza maoni ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari ili kubaini mielekeo yao kuhusu lugha ya Sheng katika kutekeleza sera ya lugha kama ilivyojitokeza katika Katiba ya Kenya ya mwaka wa 2010.

Watafiti wa baadaye waliotumia mbinu ya mlinganuo-fiche, walipata kwamba wazungumzaji walitathminiwa kulingana na muktadha (usomaji wa matini na usemaji wa kawaida). Hawa ni kama vile Romaine (1980). Wengine ni Cargile na Giles (1997) waliochunguza athari za matumizi ya lafudhi ya kigeni katika kutathmini usemaji wa mzungumzaji wa lugha Kijapani (anayetumia lafudhi ya kigeni). Hata hivyo, tafiti hizi

zilibua mielekeo ya watu kuhusu wazungumzaji wengine na lugha walizotumia kwa kusikiliza tu sauti zao bila kutazama tabia zao kuhusu lugha husika. Utafiti wetu uliegemea maoni ya moja kwa moja na kutathmini mielekeo ya watafitiwa kuhusu lugha ya Shengkama ilivyopewa nafasi katika Katiba ya Kenya.

Utafiti uliofanywa na Ihemere (2006) kuhusu lugha ya Kiikwerre na Kiingereza cha Kipijini katika jiji la Port Harcourt nchini Nigeria ulitumia mbinu ya mlinganuo-fiche. Kiikwerre hubanwa katika mazungumzo ya kinyumbani ilhali Kiingereza cha Kipijini hutumiwa katika mawanda mapana ya kijamii kama vile shuleni, kazini na katika dini ya Kikristo. Utafiti huu unatubainishia kwamba mielekeo ya watu kuhusu mtu fulani huathiriwa na lugha aizungumzayo pamoja na kiwango chake cha kijamii na kielimu. Utafiti huu wa Ihemere umetuauni si haba katika utafiti wetu kuona mielekeo waliyo nayo wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu lugha Sheng.

Mbinu ya mlinganuo-fiche katika kudhihirisha mielekeo ya watu kuhusu lugha ina mapungufu yake. Hii ni kwa sababu msikilizaji anaweza kuishia kupima usomi au usemi na pia msomaji, badala ya lugha husika. Aidha, kama asemavyo Mathooko (2007:88), tathmini inayotumia mbinu hii inaegemea sana upande wa kisaikolojia na kupuuza vipengele vingine inavyotawala maoni ya wasikilizaji kama vile kidatu cha sauti na toni ya wasomaji. Tofauti na tafiti ilizotumia mbinu hii, utafiti wetu ulitumia mbinu ya hojaji, mahojiano na utazamaji kukusanya data. Mbinu hizi zilitupa data ya moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa kwa kuwapa uhuru wa kujieleza, kwa hiyo mtafiti aliweza kufafanua maswali jambo lilosaidia katika kuondoa uwezekano wa utata upande wa maswali. Mbinu tulizotumia zimechangizana kwani ziliegemea mtazamo wa kiakili na kitabia.

Wasomi wengi nchini Kenya wanapendelea kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili katika miktadha rasmi (Ogola, 1990). Mtaalamu huyu alichunguza mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya kwa jumla. Utafiti huu wa Ogola umetufaidi si haba katika kuona jinsi maoni ya tabaka la waliosoma yalivyo kuhusu Kiswahili nchini Kenya. Walimu ni baadhi ya wasomi hivyo, mielekeo yao kuhusu suala la lugha ya Sheng imeakisi ile ya wasomi wengine nchini Kenya. Hata hivyo, mbali na utafiti wa Ogola ulioangazia mielekeo ya wasomi kwa jumla kuhusu lugha ya Kiswahili, utafiti wetu umeshughulikia wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu lugha ya Sheng kama ilivyoielezwa na kupewa nafasi katika Katiba ya Kenya. Tulitaka

kudadisi ikiwa wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari wangedhihirisha tofauti yoyote katika mielekeo yao ya lugha ya Sheng kwa sababu wao ni miongoni mwa wadau muhimu wa kimsingi katika utekelezaji sera ya lugha nchini Kenya.

Tafiti nyingine zilizotufaidi katika utafiti huu hasa katika kufahamu mbinu za moja kwa moja tulizotumia hazifai kupuuzwa. Utafiti wa Fink (2005) ulichunguza mielekeo ya watu wa jiji la Nairobi kuhusu lugha. Watu wa majijini huwa na lugha tofautitofauti asilia. Vilevile, mtafiti huyu ametumia mbinu ya hojaji kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Daystar kukusanya data. Utafiti wa mtaalamu huyu na ule wa Githinji (2008) ulipata kwamba vijana wa jiji la Nairobi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu msimbo uliowatambulisha, Sheng. Ingawa walijitambulisha kwa msimbo huu utafiti wa Githinji ulibaini kuwa wengi wao hawakuupendelea kwa sababu kukosa usanifu. Githinji anaeleza kwamba wanajamii waweza kuwa na mielekeo inayopendelea lugha inayowatambulisha ilhali wakati huo huo wakawa na mielekeo hasi kuhusu lugha hiyo wanapolinganisha usanifu wake na usanifu wa zile lugha nyingine zinazohusiana nayo (Githinji, ibid: 132).

Utafiti wa Mukhwana (2008) ulipanua ule wa Fink (2005) kwa kuchunguza mielekeo ya watu wa miji mitatu mikuu nchini Kenya ambayo ni Nairobi, Mombasa na Kisumu. Watafiti hawa walipata kwamba katika majiji haya ya Kenya, lugha ya Kiingereza hupendelewa na wengi kama njia ya kupata ajira nzuri na kwa hiyo kuonyesha tabaka ahali la kijamii. Utafiti wa Fink na ule wa Mukhwana umetufaidi kwa kutubainishia hali ya lugha ilivyo mijini Kenya, kwamba ingawa majukumu ya lugha yamependekezewa, ni jukumu la wadau husika kupanga mikakati ifaayo ili kufaulisha mapendekezo hayo. Utafiti wa Mukhwana umefaidi sana utafiti wetu kwani umetathmini mielekeo ya watu wa mijini wenye hadhi na lugha tofautitofauti asilia ambao umeenda sambamba na wetu ulioangazia mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule za sekondari kuhusu lugha ya Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri inayopatikana jijini Nairobi kuliko jamii za watu wa asili tofautitofauti.

1.9. Nadharia

Nadharia ya kisaikolojia ya jamii hujikita katika sababu kuu mbili za mtu kuweza kujifunza au kudumisha matumizi ya lugha ya pili. Kwanza ni kuwa, mtu hujifunza lugha ya pili ili aweze kuukumbatia utamaduni unaokwenda na wazuungumzaji asilia wa hiyo lugha ya pili. Katika muktadha wa utafiti wetu, mtumizi wa Sheng huwa na lugha yake asilia anayoitumia nyumbani akiwa na wazazi wake. Hata hivyo, anapokutana na marika wenzake atataka kuzungumza kama wao na kuvaa kama wao.

Pili, nadharia hii hudai kuwa, mtu anapojifunza lugha ya pili, yeye hutaka kupata manufaa yanayoendana na hiyo lugha ya pili. Kihali halisi hakuna manufaa yoyote ya kijamiiyanayotokana na matumizi ya lugha ya Sheng nchini Kenya. Kwa hali hii, hiki kipengee cha pili cha ujifunzaji lugha ya pili hakitatumikizwa sana katika utafiti wetu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusiana na lugha ya Sheng.

1.10. Haipotesia

Utafiti huu utaongozwa na haipotesia zifuatazo;

- i. Kuwa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri huenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu.
- ii. Kuwa ipo miktadha fulani ya mawasiliano ambapo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao.
- iii. Kuwa mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu pamoja na wafanyikazi wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii ni hasi.
- iv. Kuwa wafanyikazi wasio walimu huchangia matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri.
- v. Ikiwa mielekeo ya wanafunzi kuhusiana na lugha ya Sheng ni hasi au chanya, kwa kuzingatia watumizi wake ambao ni wanafunzi wa shule za sekondari; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri Nairobi.

1.11. Mbinu za utafiti

Sura hii inaeleza mahali pa kufanyia utafiti na mchakato ambao umetumiwa kufanya utafiti. Hatua zinazojumuisha mbinu za utafiti, hadhira lengwa ya kutafitiwa, hatua ambazo zimetumika kupata sampuli, jinsi ya kupata data, hatua za kuchanganua data na maswala ya kimaadili ambayo yameshughulikiwa.

1.11.1.Uteuzi na maelezo kuhusu mahali pa kufanyia utafiti

Shule ya upili ya Jamhuri imeteuliwa kimaksudi kama mahali pa kufanyia utafiti kwa kuwa ni karibu na eneo asilia linaloaminika kuwa ndilo chanzo hasa cha lugha ya Sheng la 'Eastlands' (Osinde - 1987). Sehemu hii inaidadi kubwa ya wanafunzi wanaotoka katika mitaa ya mji mkuu wa Nairobi ambako lugha ya Sheng inatumiwa kwa sana. Pia tumeweza kuwa na mtagusano na kutangamana na baadhi ya wanafunzi katika shule ya Jamhuri mara

kwa mara hasa wakati wanapoelekeo nyumbani jioni baada ya masomo na kuwasikia na hata kuweza kuzungumza nao lugha ya Sheng. Shule yenyewe inapatikana katika sehemu za kati ya mji wa Nairobi kwenye barabara kuu ya Thika karibu na soko la Ngara mwanzo wa barabara ya Limuru.

1.11.2. Idadi ya hadhira ya kafanyiwa utafiti

Kombo na Tromp (2010; pp.76) wanaeleza kuwa jumla ya hadhira inayotafitiwa ni kundi la watu au vitu vitakavyotumiwa kupata sampuli. Hadhira lengwa katika utafiti huu unajumuisha wanafunzi wa kidato cha kwanza, pili, tatu na nne kwa kuchagua angalau wanafunzi kumi kutoka katika kila kidato na pia walimu sita na wa jinsia zote wa lugha, haswa Kiswahili shuleni humo. Hii imeweza kutusaidia kupata maoni tofauti tofauti na pia kuweza kuona iwapo kuna tofauti au usawa wa maoni katika viwango hivi tofautitofauti. Wadau wengine wa shule hii wapatao kumi na ambao hutagusana kwa ukaribu na wanafunzi wametumiwa katika ukusanyaji data kwa ajili ya utafiti huu. Wahasibu, wapishi na mabawabu ndio waliolengwa hasa. Vile vile, wazazi wa wanafunzi hawa waliokuwa radhi kutumika katika huu utafiti ambao ni kumi walihusishwa. Tunaamini kwamba jumla ya watafitiwa sitini na sita ni idadi inayoweza kutupa data ya kuaminika kwa ajili ya utafiti huu na ambayo inaweza kuchanganuliwa kirahisi bila kujiingiza katika teknolojia ya kompyuta inayobadilika kila uchao.

1.11.3. Mchakato wa kuteua sampuli

Kombo na Tromb (2010; pp.77) wanaeleza kuwa uteuzi wa sampuli ni mchakato ambao mtafiti anatumia kukusanya watu, mahali au vitu vya kutafitiwa. Umuhimu wa uteuzi wa sampuli ni kupata idadi fulani ya watu wa kutafitiwa hivi kwamba wale watakaoteuliwa watawakilisha jumla ya watu wengi katika eneo husika (Mugenda na Mugenda; 2003)

Ili kupata kundi wakilishi kutoka jamii pana (wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri) tunayojishughulisha nayo, tumezingatia uteuzi wa sampuli wa mtabakisho katika hatua ya kwanza. Kufanya huku kumetuwezesha kupata vijisehemu vilivyo kundi wakilishi. Kwa muktadha huu, vijisehemu hivi vitajumuisha vidato vyote katika shule ya upili ya Jamhuri. Hatua itakayofuatia katika uteuzi wa sampuli itakuwa uteuzi wa sampuli kimaksudi. Hatua hii itatusaidia kupata walengwa binafsi ili kuwahoji. Kwa kuwa ya wingi wao, tumeteua tu walengwasitini na sita kutoka kwa wanafunzi, walimu, wazazi na wafanyikazi wa shule wasio walimu. Isipokuwa wanafunzi ambao wote ni wa jinsia ya

kiume, wazazi, walimu na wafanyikazi wa shule wasio walimu tumezingatia usawa wa kijinsia ambapo tumeteua kumi na tatu wa kike na kumi na tatu wa kiume.

1.11.4. Asili ya data

Utafiti huu umetumia ujumbe unaopatikana kwenye vitabu vilivyoandikwa na hata kutoka kwa watu waliohojiwa moja kwa moja. Data ya sekondari imepatikana kwenye vitabu vya Kiswahili na hata miongozo ambayo imewahi kuandikwa.

Watakaohojiwa ni wanafunzi ambao watakuwa wameteuliwa kama sampuli na baadhi ya walimu, wazazi na pia wafanyikazi wasio walimu katika shule ya upili ya Jamhuri.

1.11.5. Ukusanyaji wa data na vifaa vitakavyotumiwa

Utafiti umetumia hojaji zinazosheheni maswali funge na wazi. Hojaji zenyewe zimejazwa na wanafunzi na hata walimu watakaoteuliwa. Maswali funge ambayo yametumiwa sana yamesaidia kupata ujumbe ambao utafanana kutoka wahusika wote hivyo kurahisisha uchanganuzi wa data.

Vilevile mahojiano yametumika ambapo tumepata kuwauliza maswali wanafunzi katika viwango tofauti tofauti na pia walimu, hasa walimu wa lugha shuleni humo kwani wao mara kwa mara wanakumbana na hali hii ambapo wanafunzi wanatumia lugha ya Sheng katika kujieleza darasani wanapojibu maswali na hata katika kuandika majibu yao wakati wa mtihani.

Maswali ibuka pia yameulizwa wahojiwa hasa pale ambapo wametoa hoja ambazo hazieleweki moja kwa moja. Maswali kamahaya yamewachochea kusema hata zaidi kuhusu kipengee walichokuwa wameulizwa.

1.11.6. Maswala ya kimaadili

Idhini ya kufanya utafiti katika shule yenyewe imetolewa na mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Jamhuri. Vile vile wadau wa shule yenyewe wamepata kujulishwa na mwalimu hivyo kupata ruhusa. Vilevile, tumepewa idhini ya wahusika ambao wamejaza hojaji ili wapate kujiandalia shughuli yenyewe vilivyo hivyo kutoa taarifa mwafaka. Pia, tumewahakikishia wahojiwa kuwa jumbe ambazo wametoa zitakuwa za siri hivyo wasije kuhofia kuwa wangeandamwa baadaye na sheria kali. Ili kudumisha zaidi siri, majina ya waliojaza hojaji zozote hazijaandikwa mahali popote na kuwa ujumbe ambao wamepeana haujachapishwa mahali popote pale bila ufahamu na idhini yao.

1.11.7. Uchanganuzi wa data

Kutokana na data ambayo tumekusanya, tumeweza kuitia katika mafungu mbalimbali yanayoonyesha hali ya kulandana kabla ya kuichanganua. Katika uchanganuzi wetu, tumetumia mbinu sahili za kitakwimu na kisha kuonyesha matokeo haya kwa matumizi ya pai chati, grafu na hata asilimia ili kurahisishia wasomaji ufasiri wa matokeo husika. Vile vile tumeweza kutoa maelezo kwa njia ya mjadala kuhusiana na data ambayo tunaichanganua.

SURA YA PILI

MIELEKEO KATIKA SERA YA LUGHANCHINI KENYA KUFIKIA SASA

2.1. Utangulizi

Sura hii inaangazia mielekeo ya lugha kihistoria ili tuwe na msingi dhabiti kuhusu suala zima la mielekeo ya lugha nchini Kenya. Uelewa huu wa kihistoria umetuwezesha kujimegea kitengo cha mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri jijini Nairobi, kuhusu mielekeo yao kama inavyojitokeza kuhusiana na lugha ya Sheng katika sura zinazofuatia. Kihistoria mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha mbalimbali nchini Kenya kutokana na mielekeo yao kuhusu lugha wanazozifahamu na zile wanazozizungumza. Ili kujua mielekeo kuhusu suala la lugha kamasuala muhimu lililoangaziwa katika katiba ya nchi ya Kenya (2010), ni muhimu kuangazia mielekeo ya Wakenya kwa jumla kuhusu majukumu yaliyopewa lugha kutoka enzi za ukoloni hadi leo nchini Kenya na namna majukumu haya ya lugha yanavyowafikirisha Wakenya na kuwafanya wawe na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha husika. Mielekeo ya watu huchochea namna wanavyoelekezwa katika kutumia lugha tofautitofautina kuzienzi au kuzichukia. Tumetumia mielekeo hii katika utafiti huu kama msingi wa kuelewa historia ya sera ya lugha nchini Kenya na kujua kiini cha mielekeo waliyo nayowanafunzi na wadau wengine watafitiwa wa shule ya sekondari ya Jamhuri kuhusu lugha ya Sheng nchini Kenya. Haya yamefanyika kwa kurejelea suala la upangaji lugha nchini Kenya. Tumeangazia mielekeo iliyotokana na namna Wakenya walivyotumia lugha tofautitofauti kutekeleza majukumu tofautitofauti katika enzi ya utawala wa kikoloni na baada ya ukoloni. Kwa kufanya hivyo tunafahamu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusiana na utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya lugha kutokana na hadhi na umuhimu uliopewa lugha za Wakenya wakati wa ukoloni na baada ya kupata uhuru.

2.2. Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya kihistoria

Mielekeo kuhusu majukumu na matumizi ya lugha katika utafiti huu ni dhana inayohusiana na mabadiliko katika mahusiano ya kijamii miongoni mwa watu wanaowasiliana kutegemea teuzi zao za lugha fulani dhidi ya lugha nyingine kwa manufaa fulani. Mielekeo hushawishi teuzi na miitikio ya watu kuhusu lugha zao na vile vile kuhusu lugha za wazungumzaji wengine. Ili kuweza kufahamu kiini cha mielekeo ya sasa kuhusu lugha miongoni mwa baadhi ya wanafunzi nawadau wengine wa shule za sekondari na utekelezaji wa sera ya

lugha nchini Kenya, ni muhimu kuangazia mielekeo kuhusu lugha nyakati za ukoloni na baada ya ukoloni nchini Kenya, (Kembo - Sure 2002).

2.2.1. Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya enzi ya ukoloni

Mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu majukumu na matumizi ya lugha tofautitofauti nchini Kenya yanaweza kuathiriwa na kuwa chanya au hasi kutokana na sera ya lugha iliyokuweco nchini Kenya nyakati za ukoloni. Kuna thamani kubwa inayobebwa na kipindi cha ukoloni nchini Kenya kuhusiana na historia ya sera ya lugha na majukumu yaliyopewa lugha mbalimbali nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Chiraghdin na Mnyampala, 1977:54 wanasema kuwa, wamishenari wa awali wa dini ya Kikristo wakiongozwa na Dkt. J.L. Kraft na kasisi Steere walijitahidi sana kuendeleza lugha ya Kiswahili kwa kutunga makamusi na vitabu vya sarufi ya Kiswahili na pia vitabu vya kufunzia injili katika lugha ya Kiswahili. Kwa mamishenari hawa, walikuwa na mwelekeo kuwa, lugha ya Kiswahili ingewawezesha kutagusana na Waafrika na kusambaza dini ya Kikristo kwa Wakenya na pia elimu.

Hata hivyo, wamishenari hawa baadaye walikuwa na mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hii ilitokana na sababu kwamba Kiswahili kilihusishwa na lugha ya Kiarabu na kwa hivyo dini ya Kiislamu, iliyokuwa inaenezwa na Waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki kabla ya kuja kwa Wazungu. Wamishenari hawa walikipingakiswahili kwa kuamini kuwa kilikuwa lahaja ya Kiarabu (Mbaabu, 1991:8), kwa kutilia mkazo matumizi ya lugha ya kienyenji katika kueneza dini ya Kikristo nchini Kenya.

Kupitia Tume ya Elimu Afrika Mashariki (Tume ya Beecher ya 1942-1948), lugha ya Kiswahili ilipigwa marufuku katika shughuli za kimishenari za kueneza dini ya Kikristo kwa Waafrika (Mazrui 1978:228). Mwelekeo huu ulisababishwa na ukweli kwamba Waswahili wengi walikuwa Waislamu na lugha ya Kiswahili ilikuwa imeomba baadhi ya msamiati kutoka lugha ya Kiarabu. Hivyo basi wamishenari walikihusisha Kiswahili na dini ya Kiislamu. Wamishenari walianzisha shule ambamo Kiingereza kingefundishwa kama somo na Kiswahili kingetumiwa kufundishia masomo mengine. Walipendekeza lugha za kiasili ziweze kutumika kufundishia katika madarasa ya mwanzo mwanzo kisha Kiswahili kifuatie (Mbaabu, 1996:5-6).

Karne ya kumi na tisa ndiyo iliyokuwa msingi wa uundaji wa sera ya lugha Kenya katika enzi ya ukoloni. Hata hivyo, ilikuwa vigumu kwa wamishenari kutumia lugha za kiasili kuendelezashughuli za kueneza dini ya Kikristo na pia elimu. Kwa mfano, Kongamano la Muungano wa Wamishenari (The United Missionary Conference) la mwaka wa (1901) lilishindwa kutumia lugha hizi. Kwa hivyo, lugha iliyowafaa katika shughuli hizi mbili ikawa Kiswahili (Muthiani 1986).

Kanuni za maandishi na matumizi ya lugha ya Kiswahili zilianza kupangwa kwa mchango wawamishenari kama vile Askofu Steere, Ludwig Krapf na John Rebmann, ambao walifanya uchunguzi kuhusu lugha ya Kiswahili hatua kwa hatua (Mbaabu 1991:8). Kulianzishwa asasi za kimishenari ambazo zilikuwa vituo vya kibiashara, kielimu na vilevile kimatibabu (Mukhwana, 2008). Msamiati wa Kiswahili uliendelezwa kwa kasi hasa katika asasi hizo. Ingawa hapo awali istilahi za Kiswahili zilikuwa zikifafanuliwa na wenyeji wa lugha hii, mielekeo chanya waliyokuwa nayo wamishenari Wakristo kuhusu lugha ya Kiswahili iliwawezesha kuchangia katika ukuzaji wa msamiati wa lugha hii, ingawa wao walikuwa wageni. Kutokana na mwelekeo chanya wa wamishenari kuhusu lugha ya Kiswahili, makamusi na vitabu vingi vya sarufi ya Kiswahili viliandikwa. Hili liliwawezesha wamishenari hawa kuendeleza matumizi ya lugha hii ya Kiswahili, hivyo kuinuliwa kwa hadhi ya lugha hii ya Kiswahili..

Licha ya mchango wa wamishenari wa kukuza na kuendeleza Kiswahili, kulikuwa na mapungufu katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili, jambo lililosababisha mielekeo hasi miongoni mwa Waswahili na wamishenari wa jamii tofautofauti kwa sababu ya maendeleo tofautitofauti ya Kiswahili na usanifishaji upya. Wamishenari walitofautiana kuhusu lahaja bora ya kutumiwa katika usanifishaji wa Kiswahili. Isitoshe, sajili iliyohusishwa ilikuwa ya dini ya Kikristo, hivyo Waswahili wengi waliokuwa Waislamu wakawa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili (Mbaabu, 1991:9-19).

Mielekeo ya serikali ya Waingereza ilitofautiana mara kwa mara na ile ya wamishenari kuhusu lugha mwafaka za kutumiwa kutekelezea majukumu ya kielimu. Japo wamishenari alipendelea lugha za kienyeji zitumiwe, mara nyingi watawala nao walisisitiza matumizi ya lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi, watawala hawakunua kuwa lugha itumike katika kufanikisha mawasiliano tu, bali pia koloni yao ijitegemee kiuchumi na wao wenyewe kujistawisha. Walipendelea Kiingereza kutumiwe ili waendeleze pia ukoloni wa kilugha. Serikali ya kikoloni haikuwa na sera maalumu kuhusu lugha. Baadhi ya watawala, kama vile

Mkuu wa Mkoa wa Pwani wa wakati huo, C. Hobley, walipendelea lugha za Kiingereza na Kiswahili zisomeshe (Gorman 1974:406). Mkurugenzi wa Elimu J.R. Orr naye alikuwa na mwelekeo kwamba ni muhimu kusomesha lugha za kienyeji. Kwake, kusomesha Kiswahili kulikuwa kupoteza wakati, kwani mwelekeo wake ulikuwa kwamba lugha ya Kiswahili haikuwa na manufaa yoyote ya kielimu. Kwa hivyo, mnamo Septemba 1919, alitoa agizo kwamba Kiingereza kisomeshe katika shule zote zilizopewa ruzuku na serikali. Madai kama haya kuhusu lugha na tamaduni za Wakenya yaliwaelekeza Wakenya kufikiri na kuamini kwamba Kiingereza ndiyo lugha bora na inayoendeleza utamaduni bora kuliko lugha za kienyeji (Jones, 1925:8).

Wakati wa ukoloni, lugha ya Kiingereza ilionewa fahari na Wakenya walio wengi. Wazazi wengine walipendelea watoto wao wafundishwe kwa lugha ya Kiingereza kwa kuamini kuwa wangepanikiwa kupata ajira nzuri. Mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza ulitokana na imani ya wazazi hawa, kwamba ingewawezesha kujiinua kiuchumi kupitia matumizi ya lugha hii ya Kiingereza. Lugha ilitumiwa kama nyenzo ya kupitishia elimu kwa Wakenya. Baadaye kamati ya kuishauri serikali kuhusu lugha za kutumiwa kutekelezea majukumu ya kielimu iliundwa.

Tume ya Phelps-Stokes ya 1924 ilipotembelea Kenya ililalamikia hali ya sera ya lugha iliyohitilafiana nchini Kenya kati ya wamishenari na maafisa wa serikali. Tume hii ilipendelea lugha kadhaa za Kiafrika (kama vile Kiswahili, Kikikuyu, Kidholuo, Kiluhya na Kinandi) zisanifishwe na zitumike katika elimu. Baadaye Mkurugenzi wa Elimu aligundua kuwa ilikuwa ghali kuchapisha vitabu vya kutosha kwa lugha za kienyeji. Kwa hivyo, alisema kwamba Kiswahili kitumike kufundishia katika shule za Kiafrika (Gorman, ibid: 412).

Baada ya vita vya pili vya dunia, Wakoloni walilegeza upendeleo wao wa Kiswahili kwa mwelekeo kwamba lugha hii ingekuwa kizuizi kati ya Kiingereza na lugha za kienyeji. Waingereza walikuwa na nia ya kukisambaza Kiingereza kwa Waafrika, hivyo walikiona Kiswahili kama kilichoweza kuleta upinzani kwa sababu kingewaunganisha Waafrika baada ya vita. Lililofuatia mwelekeo huu ni kwamba Kiswahili kiliwekwa pamoja na lugha nyingine za kienyeji. Baadaye kulikuwa na tofauti katika silabasi kwa sababu ya mafunzo kutolewa kwa lugha tofautitofauti - Kiingereza, Kiswahili na lugha asilia. Kwa hivyo, Wakenya hawakupata fursa sawa za kielimu (Mukhwana 2008:57). Hali hii iliwapa Wakenya wa wakati huo kuwa na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Sera ya kukuza lugha ya Kiingereza na kudunisha Kiswahili ilipata msingi imara baada ya ripoti ya Tume ya Beecher ya mwaka wa 1942 na ile ya 1949. Kwa mujibu wa yaliyomo katika ripoti hizi, msisitizo ulistahili kuwekwa katika ufundishaji wa lugha za kienyeji na lugha ya Kiingereza kuchukua nafasi ya lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu yalipingwa na mnamo mwaka wa 1949 tume hii ikapendekeza lugha ishirini za kienyeji zitumiwe kufundishia shule za vijijini. Kwa hali hii, inatarajiwa kuwa mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha ya Kiswahili ingekuwa hasi.

Matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia yalibanwa kwenye shule za mijini pekee. Wakenya walivyozidi kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza ndivyo walivyozidi kujifunza utamaduni wa Waingereza na kudharau utamaduni wao wa Kiafrika. Waliendelea kuiga na kuienzi mienendo ya Waingereza kwa imani ya kujiinua kiuchumi na kisiasa, kinyume na wale wasiofahamu Kiingereza. Kupitia elimu hivyo basi, Wakenya wakawa na mwelekeo chanya kuhusu Kiingereza na kuzichukia lugha zao za kienyeji.

Kutoka mwaka wa 1949, lugha za kienyeji zilifundishwa na malengo ya miaka mitatu ya kwanza shuleni yakaelezwa katika mtaala kuwa ni kujua kusoma na kuandika katika lugha za kienyeji. Sehemu ya utekelezaji wa ripoti ya Beecher ya 1942 ilikuwa kukifundisha Kiingereza kutoka darasa la tatu na kuenda juu. Kufikia 1952, Kiingereza kilifanywa kuwa lugha ya lazima ya kufundishia na kutahini mwishoni mwa ngazi ya masomo ya shule ya msingi. Kiswahili kilifanywa kuwa somo lisilotahiniwa katika shule za msingi (Mbaabu, 1991: 84). Hii ni kumaanisha kuwa kulipandwa chembe za mielekeo hasi kuhusu lugha Kiswahili na lugha nyingine asilia kwa Wakenya kutoka kwa wakuza mitaala.

Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji zilitumiwa na watawala wa kikoloni ili kuwatenganisha Waafrika na kuwapumbaza kama mpango wa kimakusudi wa kuwagawanya ili wakoloni waweze kuwatawala kwa urahisi. Sera ya lugha chini ya utawala wa kikoloni ilihakikisha kuendelea kwa mipaka ya lugha iliyowagawa Waafrika na kuwatenganisha na wananchi wenzao (Gorman, 1974: 426). Lugha za kienyeji Kenya zilifikiriwa kuwa duni ilhali Kiingereza kilipewa hadhi ya juu.

Kabla ya uhuru nchini Kenya, lugha ya Kiswahili ilitumiwa katika mawasiliano kati ya mabwana Waingereza na watumishi wao waliokuwa Waafrika. Hapa, mwelekeo uliojitokeza kuhusu lugha ulikuwa kwamba lugha ya Kiswahili haikuwa na hadhi ya juu. Kiswahili kilionekana kama lugha ya wananchi wa kawaida wasiokuwa na jukumu muhimu katika

utawala. Kiingereza nacho kilichukuliwa kama lugha ya kifahari na ya watu wenye hadhi ya juu katika jamii. Hii ilisababisha Kiingereza nchini Kenya kuonekana kama lugha ya kifahari na daraja la kupata elimu bora kwa waliobahatika kupata elimu katika lugha hii (Mukhwana 2008:60). Hata baada ya ukoloni, Wakenya wengi wameonyesha upendeleo kwa matumizi ya Kiingereza kwa sababu kimeenziwa kutoka nyakati za ukoloni. Hili ni dhihirisho la mielekeo chanya kuhusu lugha hii ambayo imekuwa lugha rasmi kutoka kuja kwa wakoloni hadi leo.

Nchini Kenya, wakati wa ukoloni, Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji zilitumika kama lugha za mawasiliano kati ya watawala na watawaliwa na miongoni mwa wenyeji wa lugha hizi. Kiingereza kilichukuliwa na Wakenya kama njia ya kusaidia kupata madaraka wakati wa ukoloni. Kwa mujibu wa Chiraghdin na Mnyampala (1977), Wakenya walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji kwa sababu kadhaa ambazo walizitoa kama tunavyoziangazia;

Sababu ya kwanza ilikuwa kuwa, lugha ya Kiingereza Kenya ilihusishwa na tabaka la wasomi na watawala ambao walienziwa kuliko wale wasiosoma kwa lugha hii. Hii ilitumika kama kigezo cha kuwatangamanisha watu fulani na vile vile kuwatenga wengine kwa kuzingatia iwapo mtu alifahamu lugha ya Kiingereza au la. Sababu ya pili nayo ilikwa kwamba Kiingereza kilichukuliwa kama daraja la kupata elimu na kujiinua kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ina maana kuwa nchini Kenya, lugha hii ilihusishwa na kazi nzuri na vyeo muhimu katika utawala, kanisani na katika biashara. Vyeo hivi vilikuwa vya Wakenya waliokuwa wamesomana hivyo basi Wakenya wengi kufungiwa nje ya kazi zingine ambazo zilizingatiwa kuwa bora zaidi kutokana na kutojua kwa lugha ya Kiingereza.

Vile vile, walitoa sababu nyingine kuwa, Wakenya walikuwa wameelekezwa na wakoloni kuchukulia lugha zao za kienyeji kama zilizokosa ustaarabu, hivyo hazikustahili kutumika katika elimu na hata shughuli rasmi za kila siku. Hili lilichochea mielekeo hasi kuhusu lugha hizo. Hili lilisababishia Wakenya wengi kuichangamkia lugha ya Kiingereza hata zaidi ili wachukuliwe kama walio na ustaarabu. Sababu ya nne waliotoa ili kuzidhalilisha hata zaidi lugha Kiswahili na kienyeji ni kwamba, lugha za kienyeji kama vile Kiswahili zilisanifishwa na Wazungu ambao walikuwa wa asili za Kiingereza na Kijerumani. Jambo hili lilisababisha utata kwa wenyeji wa lugha na lahaja tofautitofauti, wakazona lugha zao kama zenye ugumu kusoma kwa sababu ya tofauti katika othografia, sarufi na matamshi.

Kwa kuongezea, wakuu wa shule na walimu waliwazuia wanafunzi dhidi ya kuwasiliana kwa lugha zao asilia. Waliokiuka sheria hii (waliotumia lugha zao asilia shuleni) waliadhibiwa kwa kubebeshwa mabango yalichoandikwa kwa mfano: “*I am a fool*”, au “*I don’t know English*” Yaani “*Mimi ni mjinga*”, au “*Sijui Kiingereza*” (wa Thiong’o 1986:11). Adhabu hii ilikuwa ya kufedhehesha kwa wanafunzi kama hawa, hivyo wakawa wamechukia kuwasiliana kwa lugha zao za asilia wakiwa shuleni. Matokeo yake ni kuwa Wakenya walipendelea kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza ili wasifedheheshwe kwa kuzungumza lugha zao za kienyeji. Hili linadhihirisha mielekeo hasi ya Wakenya dhidi ya lugha zao za kienyeji na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza wakati wa ukoloni. Mielekeo hii ilisababishwa na mfumo wa elimu uliokuwepo wakati huo.

2.2.2. Mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya baada ya ukoloni

Hata ingawa Wakenya wengi walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza wakati wa ukoloni, baadaye Wakenya wasomi waliitumia lugha hii kuanzisha mapinduzi. Kupitia masomo kwa lugha ya Kiingereza, Wakenya waligundua hila za utawala wa kikoloni. Walianza kutafuta juhudi ya kuwaunganisha na wenzao kama jamii yenye maadili sawa kinyume na walivyochukuliwa na wakoloni.

Wakenya waliopata elimu walipata ari ya kujitawala na kusahau walichofaidi kutokana na kuenzi lugha ya Waingereza. Kwa hivyo wao walitafuta uhuru wa kilugha ili waweze kujipatia uhuru wa kisiasa. Kiswahili kilichukuliwa kama lugha ya kuwaunganisha wakenya na kupigania uhuru wao. Aliyekuwa Rais wa kwanza wa Kenya, hayati Jomo Kenyatta, alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa baada ya uhuru. Hili lililenga kuchochea Wakenya kuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kama kiunganishi na kitambulisho cha jamii ya Wakenya. Hata hivyo, hakukuwa na sera au sheria iliyoandikwa kufafanua jinsi majukumu hayo ya lugha nchini Kenya yalivyofaa kutekelezwa kupitia sekta ya elimu (Kibiwott 2006:3).

Taifa huru la Kenya lilirithi asasi za kielimu, kisiasa, kiuchuni na kisheria kutoka katika kipindi cha ukoloni. Kupitia urithi wa asasi hizi, Kenya ilijipata ikirithi pia lugha ya watawala wao iliyokuwa ni lugha ya kikoloni na hivyo kuichukulia Kiingereza, kama lugha yake rasmi. Baada ya Kenya kupata uhuru, lugha ya Kiingereza ilichukua nafasi ya lugha rasmi na Kiswahili kikawa lugha ya taifa la Kenya. Kaida za kikoloni za kuchunguza namna ambavyo sera za lugha zingeundwa hazikuvunjwa ingawa

Kenya ilipata uhuru. Mtazamo wa kikoloni uliendelezwa kwa kukipa Kiingereza hadhi ya juu na kukitweza Kiswahili na lugha nyingine za kiasili. Kiingereza kiliendelea kuwa lugha rasmi katika Kenya huru (Mbaabu 1996: 58). Mwelekeo uliojidhihirisha dhidi ya lugha za kiasili na Kiswahili ni hasi huku Wakenya wakidhihirisha mwelekeo chanya kuhusu Kiingereza. Kama ilivyokuwa katika enzi ya ukoloni, tume na kamati mbalimbali ziliteuliwa na serikali huru ili kuchunguza na kupendekeza mabadiliko yaliyostahili katika sera za lugha nchini Kenya. Kila tume au kamati ilikuwa na mwelekeo tofauti kuhusiana na lugha zipi na kwa vipi zilifaa kutumika katika mfumo wa elimu.

Tume ya Elimu Kenya, iliyoongozwa na Ominde S.H (1964), ilipewa jukumu lakutathmini hali ya lugha nchini Kenya na ufaafu wake katika suala la elimu. Tume hii ilitoa mapendekezo yafuatayo; kwanza, kwamba lugha za kiasili zilizokuwa maarufu katika maeneo mbalimbali zitumike katika elimu ya mwanzo ya shule za msingi. Pili, Kiswahili kitumike kama somo mwaka wa 1964 ikipendekeza matumizi ya Kiingereza nacho kama lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza katika shule za msingi mpaka chuo kikuu. Kiswahili nacho kilipendekezwa kifundishwe kama somo la lazima katika shule za msingi kwa sababu kilitumiwa kama lugha yenye umuhimu wa kuwaunganisha Wakenya na kuwa ni Lingua Franca ya kimaeneo. Pendekezo la tume hii linadhihirisha mwelekeo chanya kuhusu jukumu la Kiingereza kama lugha rasmi katika mfumo wa elimu Kenya, huku Kiswahili kikichukuliwa kama lugha yenye jukumu la kuwatambulisha Wakenya (kama lugha ya taifa).

Pendekezo la Tume ya Ominde lilikatali wakwamisingi kuwa lugha ya Kiswahili ingekuwa ngeni kwa watoto wa jamii za kiasili na zile zisizo za Kibantu kwa madai kwamba ingekuwa vigumu kuwafunza watoto lugha mbili zilizo ngeni. Aidha, maoni ya wananchi yakukitaka Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia katika shule za upili yalipuuzwa na Tume ya Ominde. Mwelekeo wa tume hii ni kwamba ingekuwa ghali kutafsiri vitabu hadi lugha ya Kiswahili, shughuli waliyodai kuwa ingekuwa matumizi mabaya ya pesa za umma. Mwelekeo huo ulichangia katika kudumaza maendeleo ya lugha hii. Vivyo hivyo inabainika kwamba mielekeo ya watawala wa Kenya huru zilienzi lugha za kiasili ila kiulinganishi iliziona kuwa si muhimu katika swala la elimu na katika utangamano wa kitaifa. Kwa upande mwingine, ijapokuwa Kiswahili kilionekana lugha muhimu katika utangamano wa kitaifa, kilitiliwa shaka na wasomi pamoja na watu ambao walitoka katika jamii zisizokuwa za Kibantu. Kiingereza kilionewa fahari na kuchangamkiwa na wakenya kwa kuwa kilikuwa ni lugha waliokuwa ni watawala wa kikoloni, watawala wapya wa Kiafrika, na wasomi waliofunza

mpaka vyuo vikuu na wa kufanya kazi kubwa kubwa serikalini. Kwa hiyo, Kiingereza kilienziwa na kutamaniwa na Wakenya wengi. Isitoshe, Kiswahili hakikutiliwa maanani katika mfumo wa elimu hasaa katika shule za msingi. Katika shule hizi, Kiswahili kilipewa vipande vitatu hivi kwa juma lakini vipindi hivyo vilitumika kufunzia masomo mengine yaliyotahiniwa. Hii ni kumaanisha kuwa Kiswahili hakikutahiniwa katika mfumo wa 7-2-2-3 na kwa hiyo, hakikujitokeza kama lugha muhimu. Hali hii iliwapa wakenya kutokithamini na kwa hiyo kuelekeza wakenya katika kuwa na mielekeo hasi kukihusu.

Ripoti ya Kamati ya Ukufunzi iliyoongozwa na mwenyekiti wa Baraza la Utumishi wa Umma, Bwana W. N. Wamalwa mwaka wa 1971, ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili ikuzwe nakuendelezwa. Hili lilizingatiwa na serikali kwa muda kisha likapuuzwa. Kamati hii ilipendekeza Kiswahili kutumiwa kama lugha ya taifa. Ili kupata ufasaha katika lugha ya Kiswahili kwa wafanyikazi wote wa umma, kamati hii ilipendekeza kwamba kozi shadidi zianzishwe katika vyuo vinavyowaandaa wafanyikazi wa utumishi wa umma. Vyuo hivyo ni kama vile Taasisi ya Utawala Kenya (KIA) na Taasisi ya Ukufunzi wa Serikali (GTI) (Ripoti ya Wamalwa 1971). Serikali iliyatekeleza mapendekezo haya kwa muda na wakayatupilia mbali baadaye. Hili lilionyesha mwelekeo wa kuchanganyikiwa ambao ulikuwa chanya na baadaye hasi wa serikali na mawakala wake kwa kupuza umuhimu unaoambatana na ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa. Hili ni suala ambalo ni kiini cha mielekeo waliyo nayo baadhi ya wadau wa utekelezaji wa sera ya lugha kama vile walimu nchini Kenya hata nyakati za leo. Hata hivyo, kwa tume ya Wamalwa kufanya utafiti na kujitokeza na mapendekezo yaliyokiona Kiswahili kama lugha iliyofaa kuendelezwa ni ithibati tosha kwamba Wakenya katika ujumla wao wanakienzi Kiswahili na mielekeo yao kukihusu ni chanya ila ni serikali iliyo na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili. Sababu moja wapo ya hali hii yaweza kufungamanishwa na suala la kubana matumizi kwa upande wa serikali hasaa kuhusu ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili unaohitaji pesa.

Kamati ya Kitaifa kuhusu malengo ya sera ya elimu iliyoongozwa na P.J Gachathi, ilipendekeza kwamba lugha tawala za maeneo ambamo shule zimejengwa zitumiwe kuwafundishia wanafunzi katika miaka mitatu ya kwanza shuleni. Lugha ya Kiswahili ilipendekezwa itumike kufundishia katika shule za mijini. Kiingereza kilipendekezwa kitumike kufundishia katika shule za miji ambamo mna mchanganyiko wa asili ya watu. Hii ilimaanisha kuwa aidha Kiingereza, Kiswahili au lugha za Kienyeji zingetumika kufundishia katika darasa la kwanza hadi la tatu nchini Kenya, kutegemea ilikokuwa shule husika.

Pendekezo jingine la kamati hii ni kwamba lugha ya Kiingereza ifundishwe kama somo kutoka darasa la kwanza na kuanzia darasa la nne Kiingereza kichukue nafasi ya lugha za Kienyeji na Kiswahili kama nyenzo ya kufundishia (Chimera 1998).

Lugha ya Kiswahili ilipendekezwa kuwa somo la lazima na la kutahiniwa mwishoni mwa masomo ya shule ya msingi. Vilevile Kiswahili kilipendekezwa kifundishwe na kutahiniwa kama somo la lazima katika kiwango cha shule ya upili. Mapendekezo haya yalidhihirisha mielekeo chanya ya wadau wasera ya lugha iliyokitambua Kiswahili kama lugha muhimu nchini Kenya kupitia mfumo wa elimu. Hata hivyo, Kiswahili kilipewa vipindi vitatu kwa wiki, ilhali Kiingereza kilipata vipindi vinane. Aidha, Kiswahili kilipendekezwa kianze kufundishwa katika daraja ya vyo vikiu na walimu wa Kiswahili waandaliwe zaidi jambo lililolengwa kuwashawishi walimu na wanafunzi kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kwa kukiona kuwa muhimu kama walivyokiona Kiingereza.

Licha ya mtazamo wa tume ya Gachathi, pendekezo la kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi na ya upili halikutekelezwa hadi mwaka wa 1985, serikali ilipoanzisha mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4. Hata hivyo, hali hii ya kucheleweshwa kutahiniwa kwa Kiswahili haifai kuchukuliwa kama mielekeo hasi ya wanaserikali kuhusu Kiswahili. Serikali ya Kenya ilihitaji muda wa kutathmini mapendekezo haya ya Gachathi na vile vile kuaandaa walimu ambao wangependishwa katika mfumo mpya wa elimu. Isitoshe, haya maoni ya Gachathi yamekaririwa na aliyekuwa waziri wa elimu katika serikali ya Uhuru Kenyatta, Bwana Kaimenyi hasa kuhusiana na matumizi ya lugha za kiasili katika kufunzia katika madarasa ya mwanzo katika shule za msingi. Hivyo basi tunaweza kusema kwa yakini kuwa, mielekeo ya Wakenya kuhusu lugha katika elimu imekuwa chanya kutokana na mapendekezo ya tume ya Gachathi. Kutilia maanani kwa kukifanya Kiswahili somo la lazima katika shule za msingi na upili nchini Kenya na kutahiniwa, kuliwafanya wanafunzi kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili.

Mnamo Aprili, 1970 Mpango wa Chama Tawala cha KANU wa kukifanya Kiswahili lugha rasmi uliibuliwa. Wakenya wote wangepungumza lugha hii wakati wowote na yeyote katika muktadha wowote, rasmi au usio rasmi. Shughuli zote za serikali zilifaa zierendeshwe kwa Kiswahili. Hata waliowania ubunge, udiwani au teuzi zozote serikalini walifaa kuongea Kiswahili kizuri na ambao wangepungumza hadhira kwa dakika zisizopungua kumi. Raia wa nje ya nchi waliotafuta uraia wa Kenya walihitajika kuonyesha, kwa maandishi au

mazungumzo, uwezo wa kutumia Kiswahili. Kushindwa kufanya hivyo kungepelekea wao kupoteza uraia waowaKikenya.

Kiswahili kilipendekezwa kipewe kipaumbele kuliko Kiingereza katika shule za msingi na za upili. Serikali iliahidi kuanzisha na kufadhili kozi na vituo vya kufundishia, kusoma na kukuza lugha ya Kiswahili katika mikoa yote na pia kujenga taasisi moja kuu ya kitaifa. Hili lililenga kushawishi watu kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kauli hizo zilikuwa za kisiasa tu na serikali haikujitolea kufuatilia pendekezo hilo, jambo lililosababisha Wakenya kuendelea kuwa na mielekeo hasi dhidi ya Kiswahili (Mbaabu, 1996:132-134). Hata hivyo, juhudi zilifanywa kukitumikiza Kiswahili katika mianda rasmi na isiyokuwa rasmi. Wanasiasa waliwahutubia wananchi kwa kutumia lugha ya Kiswahili na hili lilifanywa na rais Kenyatta wa kwanza akiwa kama kielelezo. Pili, yeyote aliyehitaji kuwa mbunge au diwani alihitaji kuwa na cheti cha kuthibitisha kuwa ana ufahamu wa Kiswahili kabla ya kuidhinishwa kuwania wadhifa huo. Katika bunge la kitaifa watu walihitari kutumia ama Kiingereza au Kiswahili na hivi ndivyo wabunge kama Mulu Mutisya na Kariuki Chotara walivyo weza kufuata mijadala katika bunge. Hati muhimu za serikali kama vile, cheti cha kuzaliwa na cha kifo pamoja na fomu za kuomba vitambulisho vya kitaifa au pasipoti vilikuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Juhudi hizi zote zilizotokana na matamshi rasmi ya chama cha KANU kuhusu lugha ya Kiswahili zilionyesha nia nzuri za serikali kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa, Kenya. Kwa misingi hii basi maoni ya Ileri Mbaabu kwamba matamko ya KANU ya 1970 yalihusu siasa tu si ya kweli. Nchini Kenya, kulichapishwa taarifa za Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa kila baada ya miaka mitano baada ya Kenya kupata uhuru. Hata hivyo, ni taarifa mbili tu ambazo ziliangazia suala la lugha.

Mipango wa maendeleo wa 1979-83 ulitaja kuanzishwa kwa Taasisi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kenya. Mbaabu (1996: 134) anaeleza kuwa taarifa ya mipango huu ilipochapishwa, Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa ushirikiano na Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta ilianza kuandaa makadirio ya mahitaji ya taasisi hiyo: vifaa na majukumu. Katika taarifa ya Mipango wa Maendeleo wa 1984-88, serikali ilitangaza kuwa ingefadhili utekelezaji wa elimu ya kujifunza kusoma na kuandika kwa watu wazima. Hili lingefanyika kupitia mafunzo kuhusu maisha ya kifamilia na afya, uraia mwema na maendeleo ya vijijini. Mipango hii inatarajiwa kuwa kishawishi cha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili miongoni mwa Wakenya, wakiwemo walimu. Hata hivyo, serikali haikufuatilia mipango hii na mwishowe

haikuanzisha taasisi iliyokusudiwa kuongoza katika utafiti, maandishi, uundaji wa msamiati na hivyo ukuzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mielekeo iliyokidunisha Kiswahili na kukitukiza Kiingereza ilibakia miongoni mwa Wakenya. Hata hivyo, ifahamike kuwa yaliyokuwemo katika mipango hii yameweza kutekelezwa hapa na pale. Kwa mfano, chuo kikuu kishiriki cha Kenyatta kilichokuwa chini ya chuo kikuu cha Nairobi hatimaye kilianzisha taasisi ya Kiswahili iliyokuwa chini ya ukurugenzi wa Profesa Ndungo. Hata ingawa taasisi hii haikudumu, hatuwezi kulaumu serikali katika ujumla wake kwa kuwa ilionyesha nia nzuri kwa kuanzisha taasisi hiyo. Nacho chuo kikuu cha Nairobi hakijasazwa katika suala zima la ukuzaji wa Kiswahili kupitia asasi mbalimbali. Kwa muda mwingi, idara ya isimu na lugha za kiafrika imekuza Kiswahili kupitia kwa kuzalisha wataalamu wa Kiswahili na vile vile kuhamasisha umma wa wakenya kukienzi Kiswahili kupitia kwa vyombo vya habari kama vile magazeti na redio. Kipindi cha ubingwa wa lugha na lugha yetu kwenye KBC redio taifa kilikuwa kikichangamkiwa na Wakenya wengi kabla ya serikali kufanya mawimbi ya utangazaji kuwa huru na kuzalisha vituo vingi vya redio. Isitoshe, chuo kikuu cha Nairobi kina idara ya Kiswahili ambayo inaendelea kuzalisha wataalamu wa lugha hii ambao wanaendelea kukuza Kiswahili nchini na katika mataifa ya ughaibuni kukiwemo Amerika, Ujerumani, Uchina na Korea. Kutokana na juhudi hizi, Wakenya hutuwa moyo wakafahamu kuwa Kiswahili kinaweza kuwalisha na kuwavisha na kwa hiyo, mielekeo ya kukihusi sio hasi.

Tume iliyoongozwa na C. B. Mackay (1981) ilipendekeza sera ya lugha iliyopendelea na kuhimili maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Tume hii pia ilipendekeza kufundishwa kwa Kiswahili katika kiwango cha vyuo vikuu. Ilipendekeza kuwa katika chuo kikuu kilichonuiwa kuanzishwa na serikali, cha Moi, kuanzishwe kitengo cha Lugha za Kiafrika kilichofaa kujumuisha Kiswahili na lugha nyingine za Wakenya katika Kitivo cha Mtalaa wa Kijamii, Utamaduni na Maendeleo. Kiswahili kilipendekezwa kuwa somo la lazima katika chuo hicho kipyua, kwa kuhoji kuwa kulikuwa na wanafunzi wengi waliohitimu elimu ya chuo kikuu lakini hawangeweza kuwasiliana kwa Kiswahili – lughaya taifa. Kufuatia pendekezo hili Idara ya Kiswahili ilianzishwa chuoni humo mwaka wa 1987. Aidha, walipendekeza Kiswahili kijumuishwe katika Somo la Mawasiliano kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza.

Kwa kuangazia mapendekezo ya Ripoti ya Mackay, tunatanabahishwa kuhusu jukumu la lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na tume hii ilinuia kujenga msingi imara wa kukikuzi na kukiendeleza Kiswahili nchini Kenya. Hatua ya serikali ya kukubali pendekezo

la kuanzisha mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambapo lugha ya Kiswahili ilifanywa somo la lazima na kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari ni muhimu katika ukuzaji wa lugha hii. Jambo hili limewahamasisha wengi kuwa na mwelekeo chanya na kukionea fahari Kiswahili na hata wataalamu kuchapisha vitabu mbalimbali kwa lugha hii ya Kiswahili. Hata hivyo, tume hii ilipendekeza kuwa lugha ya Kiingereza ibakie kama lugha ya kufundishia. Lugha za kienyeji nazo zilipendekezwa zitumike kufundishia darasa ya chini katika shule za msingi, lakini katika maeneo ambamo hili lingewezekana (Njoroge, 1990). Wakenya, wakiwemo walimu, walidhihirisha mielekeo hasi dhidi ya Kiswahili na lugha nyingine za kienyeji. Lugha za Kiafrika zilitumiwa shulenikufunzia katika madarasa ya mwanzo kama ilivyopendekezwa na tume ya Mackay. Kiswahili kilitahiniwa katika kiwango cha shule ya msingi na shule za sekondari bali na kufundishwa hata katika vyuo vikuu. Hali hii, ilijenga msingi imara wa lugha za Kiafrika Kenya, Kiswahili na hata Kiingereza kama lugha ya kimataifa. Hata hivyo, Chuo Kikuu cha Moi hakijawahi kufundisha Kiswahili kwa wanafunzi wake wa vitivo vingine kama vile, kile cha Sheria, Matibabu na Utunzaji wa Misit. Kwa hali hii, inabainika kuwa nafasi ya Kiswahili kama lugha muhimu ya mawasiliano kwa wanataaluma nchini Kenya imepuuzwa. Kwa jumla, ni chuo kikuu cha kibinafsi cha Baraton mjini Kapsabet kinacho wapa wanafunzi wake hiari ya kujifunza ama Kiswahili au Kifaransa kama lugha muhimu zinazo weza kutumika kwa mawasiliano wanapokuwa wanafanya kazi nyanjani.

2.3. Katiba ya Kenya 2010

Katiba inayotumika sasa nchini Kenya ilirekebisha, ikapendekezwa na kupitishwa na Wakenya mnamo Agosti 4, 2010. Katiba hii imeleta matumaini mapya kuhusu suala la lugha nchini Kenya. Kauli za Katiba hii zinazohusu suala la lugha nchini Kenya zinaakisi sera ya lugha inayotambua hali ya wingilugha ambayo haikutambuliwa katika katiba ya kabla ya ile ya 2010.

Kwa mujibu wa yaliyomo katika Katiba ya Kenya (Sura ya 2, Ibara ya 7), lugha ya Kiswahili kama lugha mojawapo ya lugha za Kienyeji na lugha ya taifa, imekwezwa kihadhi na kuwa pia lugha rasmi sambamba na lugha ya Kiingereza. Aidha, serikali imenuia kutunza, kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha asilia za Wakenya. Kupitia kipengee hiki, lugha ya Sheng imepata nafasi katika katiba na kuweza kuchangamkiwa na baadhi ya wananchi. Hili linatokana na Katiba mpya ya Kenya (2010) kumpa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea.

2.3.1 Sera ya lugha nchini Kenya kwa mujibu wa katiba ya Kenya 2010

Kenya ni nchi iliyo na zaidi ya lugha 40 zinazozungumzwa na watu wa makabila tofautitofauti (Abdulaziz, 1982). Maelekezo ya Katiba ya Kenya ya 2010 yanaangazia hali hii ya wingilugha, nchini Kenya. Kuteuliwa kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na kuongezewa jukumu la kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza kunadhihirisha kuwa ofisi zote za kiserikali na vilevile zile zinazohudumia umma zinafaa kuzingatia kauli hii ya Katiba. Hii ina maana kuwa lugha hizi mbili zitatumika katika mawasiliano rasmi kati ya maafisa wa umma na wananchi katika kiwango cha kitaifa na pia majimboni. Mazungumzo rasmi hivyo basi yanaweza kufanywa kwa lugha rasmi au lugha asilia inayopendelewa na hadhira lengwa hasa katika majimbo husika. Jitihada za kutoa nyenzo za kutafsiri zitafanywa kama zilivyoahidiwa katika katiba (Jamhuri ya Kenya, 2013:28). Ili kuhakikisha utekelezaji wa sera inayohusishwa na lugha rasmi, serikali ya Kenya imeanza kubuni mikakati ya kuhakikisha kuwa Wakenya wamebadili mtindo wa kutumia Kiingereza katika ofisi za serikali na asasi za elimu. Hili litakiwezesha Kiswahili kutumika katika miktadha sawia na Kiingereza (Jamhuri ya Kenya, 2013:25). Serikali ya Kenya mnamo mwaka wa 2018 imetangaza kubuniwa kwa baraza la Kiswahili la taifa na kwa sasa baraza hili limeanza kazi chini ya wasomi wa Kiswahili akiwemo Clara Momanyi. Mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi inatarajiwa kudhihirika miongoni mwa Wakenya kufuatia mikakati hii mwafaka inayotekelezwa na serikali.

Katiba ya Kenya (2010) imetaja kwamba matumizi ya lugha asilia za Wakenya yatalindwa, kukuzwa na kuendelezwa. Kauli hii inazingatia haki za matumizi ya lugha kama zinavyoelezwa katika Azimio-Bia la Haki za Matumizi ya Lugha (UNESCO, 1998) na ambazo ni Haki za Kibinadamu. Kwa kuangazia suala la haki za matumizi ya lugha, serikali ya Kenya haina budi kubuni njia za kuhakikisha kuwa kila Mkenya amehudumiwa kwa kutumia lugha anayoielewa inapohitajika (Jamhuri ya Kenya, 2013:12). Jambo hili litavutia mielekeo chanya kuhusu lugha zao asilia, jambo ambalo halikutokea kabla ya kuidhinishwa kwa Katiba ya mwaka wa 2010. Jambo la kutia moyo ni kwamba, katika mahakama za Kenya, huduma zaukalimani hutolewa kwa washukiwa na washitaki wasiofahamu lugha kuu za mahakama ambazo ni Kiingereza na Kiswahili. Mwalimu Lukaka wa chuo kikuu cha Nairobi hushiriki katika huduma hii hasa wanaohusika wanapokuwa ni Machina kwa sababu ya ufahamu wake wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kichina.

Kutokana na kauli ambazo tumejadili hapo juu kuhusiana na suala la lugha katika Katiba ya Kenya ya 2010, swali tunalouliza ni je, ni ipi mielekeo ya wanafunzina wadau wa shule za sekondari kuhusu kauli hizi za Katiba zinazohusiana na matumizi ya lugha nchini Kenya? Wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari hawa wana mielekeo inayokubali au isiyokubali kauli kama hizi za Katiba ya Kenya hasa kuhusiana na lugha pendwa ya vijana nchini Kenya ya Sheng? Wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari wana mistakabala ipi kuhusu lugha ya Sheng ikizingatiwa kuwa Katiba mpya ya Kenya (2010) imempa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea? Ili kupata majibu ya maswali haya, tumeweza kuangazia majibu ambayo tumepokea kutoka kwa wahojiwa ambao wamejaza hojaji na wale tumekuwa na mahojiano ya moja kwa moja na wao.

2.4. Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili suala la mielekeo ya Wakenya kuhusu matumizi ya lugha nchini Kenya kutoka enzi ya ukoloni hadi sasa. Tumeangazia nafasi ya serikali ya kikoloni katika kuathiri namna ambavyo watu wamekumbatia lugha tofautitofauti nchini Kenya. Kwa kusema hivi tuna matarajio kwamba matumizi ya lugha fulani katika kutekeleza majukumu fulani yameshawishi Wakenya, kwa njia chanya au hasi, kuwa na mielekeo fulani kuhusu lugha husika. Kiingereza kimeenziwa kama lugha rasmi nchini Kenya kutoka enzi ya utawala wa mkoloni. Wakenya walikienzi Kiingereza kwa sababu lugha hii ilichukuliwa kama daraja la kupata ajira bora na kujiinua kiuchumi. Lugha ya Kiswahili, kimejitokeza kama lugha muhimu katika mawasiliano ya kitaifa tokea enzi ya ukoloni hadi sasa. Lugha hii hufunzwa na kutahiniwa katika ngazi mbalimbali za elimukenya na ni lugha ya taifa. Kutokana na katiba mpya ya Kenya (2010) Kiswahili ni lugha ya kwanza rasmi Kenya japo nafasi ya Kiingereza haijaathiriwa na kauli hii. Lugha za Kienyeji nazo zinachukuliwa kama lugha za mawasiliano ya kikabila nchini Kenya. Kwa hivyo, lugha za kienyeji hazijafaa kutumika katika elimu ya juu isipokuwa Kiswahili kinachofunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na sekondari. Wakenya wengi wameishia kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiingereza na mielekeo hasi kuhusu lugha zao asilia.

Ingawa hali ya lugha katika utawala wa kikoloni iliathiri mielekeo waliyokuwa nayo Wakenya hata baada ya uhuru, Katiba ya Kenya iliyopitishwa mnamo Agosti, 2010 imeleta matumaini mapya nchini kwa sababu serikaliimewezakuzitambua na kunuia kukuza na kuendeleza matumizi ya lugha na tamaduni tofautitofauti za Wakenya. Hata hivyo, hofu

iliyopo ni kwamba huenda kauli hizi zipuuzwe kama ilivyokuwa awali na Wakenya waendeleo kupata mielekeo ya jadi kuhusu lugha mbalimbali.

Jambo hili lili ndilo limetupelekea kutafiti na kutaka kujua kwa zaidi kuhusu suala la mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu Sheng kama ilivyojitokeza katika Katiba ya Kenya 2010 na kujua namna ambavyo wanaichangamkia lugha hii ya Sheng, iwapo mielekeo yao ni chanya au hasi.

SURA YA TATU

MATOKEO YA UTAFITI

3.1. Utangulizi

Sura hii inashughulikia matokeo ya utafiti wetu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusu Sheng katika shule za sekondari; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, mjini Nairobi kwa kuweza kuangazia majibu kutokana na hojaji ambapo tuliwashirikisha wanafunzi katika vidato vyote vinne, walimu, wafanyikazi wasio walimu na wazazi wa wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri kwa lengo la kutaka kufahamu na kubainisha ikiwa kuna muoano wowote katika mielekeo ya wote ambao wameshirikishwa katika utafiti huu.

3.2. Matokeo ya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau kuhusu Sheng

Baada ya hojaji kuwasilishwa, kujazwa na kisha kurejeshwa tumeweza kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wahojiwa wetu ambayo tumeweza kuyawasilisha kwa viwango mbalimbali kwa kuzingatia maswali katika hojaji hizo. Kwa kuwa hojaji zenyewe zimegawika katika sehemu kumi natisa (maswali kumi na tisa), tumeangazia matokeo yake kulingana na kila moja wapo ya maswali ili kupata maoni ya kila mshiriki ambayo yametupa mwanga kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau kuhusu Sheng. Kwa kuwa washiriki walikuwa wa aina nne tofauti yaani, wanafunzi, walimu, wafanyakazi wasio walimu na wazazi, tumeweza kutenga vijishehemu hivi vinne na kuangazia maoni ya kila kikundi cha uhusika kwa hali yake kabla ya kutoa maoni yao kwa ujumla kama hitimisho.

3.2.1. Wanafunzi

Tumeanza kwa maoni ya wanafunzi ambao tumewahoji kwa kuzingatia maswali kumi na tisa ambayo tumewauliza katika hojaji zao. Baada ya kupokea hojaji zilizokuwa zimejazwa, tumepata kugundua kuwa washiriki wetu wa umri kati ya miaka kumi na minne hadi miaka kumi na minane ndio wanaopatikana kati ya kidato cha kwanza hadi kidato cha nne. Wahojiwa arubaini kwa jumla huku shughuli ya upataji data ikishirikisha wanafunzi kumi kutoka kila kidato.

Kwa kuzingatia miaka ambayo wahusika hawa wamekuwa katika shule hii, tumepata kufahamu kuwa wale wa vidato vya juu, yaani kidato cha tatu na nne, wamedhihirisha wazi kuenzi na kuchangamkia lugha ya Sheng kwasana. Hata baada ya kuwa na mahojiano ya moja kwa moja na baadhi yao, tumepata kujua kuwa wanaipendelea lugha ya Sheng kwa

mazungumzo yao ya kila siku wakiwa shuleni na hata nyumbani. Sababu yao ya kimsingi ilikuwa kwamba, Sheng inawasaidia kuficha siri nyingi kutoka kwa wakubwa zao ambao mara nyingi hawakutakiwa kushirikishwa au kuelewa kile wahusika hawa wanazungumzia au kujadiliana. Hata hivyo katika swali la tano katika hojaji yetu, tumegundua kuwa takribani asilimia sitini ya wasailiwa iliweza kuitaja lugha ya Sheng kama mojawapo ya lugha wanazozifahamu. Hili lilikuwa dhahirisho kuwa wahusika wana mielekeo chanya kuhusiana na lugha hii ya Sheng na hii ndio maana ya wao kuweza kuipendelea lugha hii katika mawasiliano yao ya kila siku.

Hata baada ya kuwapa wanafunzi hawa hojaji bila kuwauliza sehemu wanakoishi mjini Nairobi, tuligundua baadaye kuwa wanafunzi wengi katika shule ya upili ya Jamhuri wanaishi katika mitaa ya “Eastlands” ambakokwa mujibu wa Bulibu na wenzake (2006) wanasema kuwa Sheng hutokana na mwingiliano wa vijana wa makabila mbalimbali wanaopatikana katika mitaa ya Huruma, Mathare na hata Kaloleni ambayo ipo “Eastlands”. Vile vile, maoni yake Gathiora (2002) yanakumbatiwa hapa kwani kutokana nabaadhi ya hojaji tumepata kuona kuwa washiriki ambao wamejaza wanatoka katika mitaa ya Kangemi, Kwangware na hata Githurai sawia na madai yake Gathiora kuwa Sheng ilianza kule nah ii ni ishara kuwa utafiti huu umedhahirisha maoni yake kuwa ya kweli.

Katika swali la tano katika hojaji zetu, tumeweza kuungama na maoni yake Abdulaziz na Osinde (1997) ambao wameelezea chimbuko la Sheng kwa kusema kuwa ilitokea katika mwaka ya (1963) baada ya uhuru ambapo watu wengi walihamia mijini kwa sababu yakutafuta kazi na kuweza kuishi katika mitaa au jamii ya utatu lugha na ndiposa kukazuka lugha ya Sheng. Maoni haya yameweza kuwiana na majibu kwa swali la tano katika hojaji zetu ambapo wahusika wameulizwa kutaja lugha wanazozifahamu na kwa hakika wakataja lugha zao za kienyeji, Kiswahili na Kiingereza kama yalivyo maoni ya waandishi hawa. Pia mwandishi Buliba na wenzake (2006) anasema kuwa Sheng hutokana na mwingiliano wa vijana wa makabila mbalimbali ambayo ni kweli kwani wahusika ambao wanashiriki katika kujaza hojaji hizi ni wa makabila mbalimbali lakini kutoka katika mitaa sawa mjini Nairobi kuashiria kuwa kuna mwingiliano kati yao.

Washiriki wetu ambao ni wanafunzi wameulizwa iwapo Sheng ni lugha katika swali la sita katika hojaji ambazo tumewapa, wengi wao, karibu asilimia tisini wanasema ndio na kwamba wao huitumia sana katika mawasiliano. Hii pia imekuwa ishara tosha kuwa wanafunzi hawa wanaienzi lugha ya Sheng na kuwa na mielekeo chanya kuhusu Sheng.

Imedhihirika wazi pia kuwa wanafunzi hawa hutumia Sheng hasa na marika wenzao na sababu kuu ikiwa ni kuficha maana kutoka kwa kundi ambalo sio la umri wao na pia kama kitambulisho cha kundi fulani lililo na mawazo na fikra sawa kuhusiana na hali yao ya maisha. Matumizi haya ya Sheng hutokea mahali popote mradi tu vijana hawa wapo pamoja. Hivyo basi, vijana huichangamkia lugha ya Sheng mahali popote mradi wawe na wenzao wanaoelewana na kuweza kuwasiliana.

Alipoulizwa iwapo mwanafunzi/mshiriki hutumia Sheng akiwa shuleni, jibu ni ndio kwa wahojiwa wanafunzi thelathini kwa jumla ya arobaini tuliowahoji. Sababu zao zikiwa, wengine wao ili waweze kukubalika miongoni mwa marika wenzao na pia ili kuficha maana kutoka kwa kundi ambalo kwao wanaliita watiaji (wasio marafiki zao).

Majibu ya wanafunzi katika hojaji kuhusu swali la tisala iwapo wanapendelea Sheng au lugha ya Kiswahili sanifu, asilimia zaidi ya tisini imeitaja Sheng kama lugha inayopendelewa zaidi na kutoa maoni kuwa ni rahisi kuielewa Sheng na pia kuwa Sheng haina kanuni na sheria nyingi funge zinazofaa kuzingatiwa katika mazungumzo au matumizi yake. Pia washiriki hawa waliungama kuwa matumizi ya Sheng huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kwani wengi wao hujipata kukosa neno mwafaka la Kiswahili sanifu wakati wa mazungumzo rasmi na walimu au wakubwa zao kutokana na mazoea ya kutumia maneno ya Sheng ambayo sio sanifu. Pia katika mitihani yao, wanafunzi wengi wamejipata wakitumia maneno ya Sheng wakati wa kujibu maswali ya lugha na fasihi ya Kiswahili na pia wakati wa uandishi wa insha kwa Kiswahili. Wameungama kuwa hili limesababisha kudhororakwa matokeo ya lugha ya Kiswahili kwa kupata alama za chini sana katika mitihani wao wa Kiswahili.

Katika kutaka kujua ni jinsia gani inayopendelea sana kutumia lugha ya Sheng, zaidi ya asilimia tisini imetoa maoni yao kuwa ni jinsia zote. Sababu zao zikiwa kwamba kila jinsia katika umri huo wao wa kati ya miaka kumi na minne hadi miaka kumi na minanewanaichangamkia lugha ya Sheng katika mazungumzo yao kwani yanawawezesha kutangamana na marika zao kwa urahisi na pia kuweza kujumuishwa katika mipango mbalimbali iliyowahusu kama vijana. Ili kukubalika na kushirikishwa katika matembezi, kucheza densi kila mmoja wao anahitajika kujua na kuzungumza Sheng ili aweze kushirikishwa. Hivyo basi jinsia zote zilionekana kuchangamkia Sheng katika mazungumzo na shughuli zao za kila siku.

Kuhusu swali la kutoathirika na Sheng hata iwapo mhusika anaishi katika mazingira wanamozungumza lugha ya Sheng kwa wahusika hawa wanafunzi, jibu lilikuwa la. Sababu zao ni kwamba ingekuwa vigumu kwa yule ambaye hangeweza kujua Sheng kwani hutengwa na wenzake katika mambo mbalimbali na kutoshirikishwa katika mipango ya wanajamii wanaozungumza lugha ya Sheng. Hivyo basi kila mmoja katika wahojiwa hujipata ameikumbatia Sheng na kuitumia katika shughuli zake za kila siku.

Mwelekeo wa mzungumzaji kuwa na mwelekeo kuhusu lugha moja iwe chanya au hasi kama swali la kumi nanne linavyouliza katika hojaji zetu limepatamajibu tofauti lakini asilimia zaidi ya hamsini imeonekana kutoa sababu zao kwa kuegemea mwelekeo chanya wa wahusika wanafunzi ambao wameshiriki. Fafanuzi zao zimekuwa kama vile, kuipendelea lugha ya Sheng kwani ni rahisi kuitumia kwani haina sheria au kanuni yoyote ya kuitumia, lugha ya Sheng huficha siri katika mazungumzo na pia kupunguza makali ya maneno fulani ambayo ni machafu au yanaweza kuzua ugomzi na hata wengine kutaja kuwa ni kitambulisho cha marika fulani na sehemu unayotoka, jambo limefanya mhusika kuwa au kupata marafiki.

Mielekeo ya wazungumzaji pia imeonekana wazi kuweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani katika mazungumzo. Kwa mujibu huu kutokana na hojaji zetu, mielekeo ya washiriki wetu ambao ni wanafunzi imeweza kuathiri uteuzi wao wa lugha ambayo ni ya Sheng katika mazungumzo yao. Kulingana nao, wanaichagua lugha wanayoipenda ili kuweza kuitumia katika mazungumzo yao. Asilimia zaidi ya tisini ya hojaji ambazo zimejazwa na wanafunzi zimeonyesha kuwa mielekeo ya mzungumzaji huathiri uteuzi wa lugha fulani kwa hali hii lugha ya Sheng na mzungumzaji. Hili linatokana nakuipendelea lugha hiyo na kuiona kuwa rahisi kuelewa na pia kuitumia katika mazungumzo yao ya kila siku.

Kama ilivyo katika swali la kumi na sita, washiriki wetu ambao ni wanafunzi walikiri ya kwamba lugha ya Sheng huathiri utendakazi wao katika masomo mengine. Sababu zao zikiwa, kuna maneno mengine ya lugha kama vile Kiingereza ambayo wameweza kuvunja sarufi zake au hata kwa wakati mwingine kuyaswahilisha na kujipata wakiyatumia katika maandishikwa hali hiyo katika masomo mengine yanayotahiniwa katika lugha ya Kiingereza.

Mazingira wanamoishi washiriki hawa wanafunzi yameweza kuchangia katika mielekeo yaokuhusiana na lugha ya Sheng kutokana na jibu la swali ya kumi na saba katika hojaji

ambazo tumewapa. Washiriki thelathini na tano wamekubaliana na kauli hii kuwa mazingira unamoishi mnachangia katika mwelekeo wa mhusika kuhusiana na lugha ya Sheng. Hii imetokana na kuogopa kusengenywa/kutoelewa kinachozungumzwa na hata kutengwa na kundi ambalo mhusika anaishi nalo na ili kuweza kuwa na ushirikiano na kutambuliwa kama mmoja wa wanajamii husika wa eneo hilo, ilimbidi mhusika huyo kujua lugha ya Sheng iwapo anaishi katika eneo ambalo kila mzungumzaji anaitumia na kuenzi lugha hiyo ya Sheng.

Iwapo mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi au wazazi pamoja na wadau wengine wa shule ni swali ambalo lilijibiwa ndio na washiriki thelathini na tano wakitoa sababu zao kuwa walimu hasa wa lugha hawapendi lugha ya Sheng na huwakashifu na hata kuwa na uhusiano unaoyumbayumba nao kwani matarajio yao ni kuwa wanafunzi watumie lugha sanifu katika mazungumzo na mawasiliano yao ya kila siku. Kwa upande mwingine maoni yao kuhusu uhusiano wao na wazazi ni kuwa lugha ya Sheng haiathiri uhusiano nao kwani wazazi wao pia hutumia lugha hii ya Sheng kutokana na mazingira wanamoishi ambapo wakazi wengi wanatumia lugha ya Sheng katika mazungumzo yao na shughuli zao za kila siku. Kwa upande wa wadau wengine kama vile wafanyikazi wa shule wasio walimu ni kuwa kuna baadhi yao ambao pia hutumia lugha hii ya Sheng kwa sababu makazi yao ni ya mitaani ambako wanafunzi hawa pia huwa, kama vile wapishi na mabawabu hivyo basi kuwa na uhusiano mwema nao isipokuwa wachache ambao wamo maofisini ambao pia hukashifu matumiazi haya ya lugha ya Sheng na kutaka kuzungumziwa kwa lugha rasmi kama vile Kiingereza au Kiswahili sanifu. Hii imetokana na wao kupokea wageni mara kwa mara kutoka nje na hivyo kuwabidi kuwa na urasmi huu.

Maoni kutokana na swali la kumi na tisa ndilo limekuwa na tetesi mbalimbali kutokana na majibu ambayo tumeyapata kutoka kwa wahojiwa wetu ambao ni wanafunzi. Wengi wao wa idadi ya washiriki thelathini wameonelea kuwa Sheng iweza kupewa kibali cha kuweza kutumiwa wazi bila ya vikwazo vyovyote vile vinavyoiona Sheng kuwa lugha ya wahuni na hata wezi. Hata hivyo, washiriki wanane nao wakatoa maoni yao kuwa, Sheng ibaki kutumiwa tu na wale wanaoifahamu katika miktadha yao kwani ni njia moja ya kuficha siri na ujumbe ili usiweze kueleweka na wasiokusudiwa kuuelewa ujumbe huo. Washiriki wawili nao hawajaweza kuelewa swali nahawajatoa jibu lolote katika swali hili. Hivyo basi imedhihirika wazi kuwa wengi wa wanafunzi wanataka kupewa uhuru wa kutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano na mazungumzo yao ya kila siku kwa uwazi.

Kutokana na maswali ya hojaji hizi tulizoandaa na kuwapa wanafunzi ili kupata maoni yao, ni dhahiri kuwa wahojiwa wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng na kuwa wanaienzi na kuitumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Maoni yao yametupa mwelekeo na mwanga zaidi kuhusiana na mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari kuhusu Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, Nairobi ambayo imetumika kama kiwakilishi cha shule zote nchini Kenya.

3.2.2. Walimu

Washiriki wengine muhimu katika utafiti huu ni walimu. Hii ni kwa sababu hawa ndio huwa na mtagusano wa kila siku na wanafunzi ambao tunawatafitia kuhusu mielekeo yao kuhusu lugha ya Sheng. Kwa kupitia hojaji ambazo tumewapa, tumeweza kupata maoni yao mbalimbali kwa kuzingatia maswali ambayo tumewauliza kuhusiana na utafiti wetu. Kwa jumla tumeandaa hojaji kwa walimu sita wa lugha kuzingatia jinsia zote, watatu wa kike na watatu wa kiume ambao umri wao ni kati ya miaka ishirini na nane hadi miaka hamsini na viwango vyao vya elimu vikiwa vyo vikuu. Maoni yao kwa maswali yetu yamekuwa kama yafuatayo;

Muda waliofunza shuleni humu ni kati ya miezi mitatu hadi miaka ishirini. Makazi yao kwa wengine pia ni mitaa ambayo lugha ya Sheng ilianza na hata kutumiaka kwa sana hadi sasa. Mitaa hii ni kama vile, Githurai na Gumba inayopatikana katika eneo la Mashariki mwa jiji kuu la Nairobi kulikoanzia na kuenea kwa lugha hii ya Sheng.

Wahojiwa wetu pia wana ufahamu wa lugha tatu (utatulugha) kwani wanaifahamu lugha yao ya Kienyeji, Kiswahili na Kiingereza. Wahojiwa wote pia wameonekana kuweza kuzifahamu lugha zao zilizowazaa na kuwalea na vile vile kuzitumia katika mawasiliano yao hasa na wenzao wanaozifahamu pia lugha hizo.

Baadhi ya walimu wamekubali kuwa Sheng ni lugha huku wengine wakikataa kuwa Sheng sio lugha. Wanaokubali kuwa Sheng ni lugha wanazidi kuelezea kuwa ndio wao huitumia lugha ya Sheng hasa wakiwa katika makazi yao wanapoenda kununua viungo kutoka kwa mama mboga na pia katika matwana wanapoelekea kazini na wanapoenda nyumbani na utingo au dereva anapowaitisha nauli au kuwaeleza utingo wawashushe iwapo wamefika wanapoelekea.

Swali kuhusu iwapo wao hutumia lugha ya Sheng wakiwa shule limeweza kukataliwa na kila mwalimu na labda kwa kuzingatia kuwa wahojiwa wote ni walimu wa lugha sababu yao

ikiwa kuwa Sheng sio lugha rasmi na kwa kuwa walimu wa lugha wanahimiza wanafunzi wao kutumia lugha ya Kiswahili sanifu ili hata kuweza kujibu maswali ya Kiswahili kwa ufasaha. Vile swali la kumi linalouliza iwapo wanapendelea lugha ya Sheng au Kiswahili sanifu, majibu yao yamekuwa ni Kiswahili sanifu na pia kutoa sababu kuwa wao wanahimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu.

Kutokana na matokeo mabaya ya mtihani wa Kiswahili, wahojiwa wote waliunga mkono kauli ya kwamba mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Makosa mengi ya matamshi yametokana na athari ya matumizi ya lugha ya Sheng na pia makosa hayo kuweza kutokea katika maandishi. Maoni yao yameweza kudhihirishwa kwani mhojiwa mmoja ametuonyesha insha moja ya mwanafunzi ambayoina makosa yanayotokana na athari ya matumizi ya lugha ya Sheng (... *nilitoka nduki...*) kwa kusudi la kutaka kusema alitoka kwa haraka. Hii ni dhahiri kuwa lugha ya Sheng inaathiri matokeo ya wanafunzi katika lugha ya Kiswahili kama swali la kumi na sita linavyouliza na maoni hayo kutolewa na walimu ambao wamejaza hojaji na hata wengine kuwa na mahojiano ya moja kwa moja nasi.

Kwa upande wa jinsia, wahojiwa hawa wametoa kauli yao kuwa ni jinsia zote hutumia na kupenda lugha hii ya Sheng. Hata ingawa wanafunzi katika shule yao ni wa kiume, wengine wao wana watoto wa kike kwao ambao wanasema kuwa wanawasikia mara kwa mara wakizungumza na wenzao kwa lugha ya Sheng. Kwa upande wa uwezekano wa kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumiwa, wahojiwa hawa wameunga mkono kauli hii kwani washiriki watanoambao wanaishi katika mitaa ambamo Sheng ilianza na kukua na hadi sasa kutumika lakini hawajaathiriwa na lugha hii ya Sheng kwa vyovyote vile.

Sababu zinazoweza kumfanya mzungumzaji kuwa namwelekeo kuhusu lugha moja hasa lugha ya Sheng kulingana na maoni ya walimu hawa ni kuwa; kwanza hadhi ya lugha hiyo katika jamii, manufaa ya lugha hiyo hasa katika upande wa elimu, kuelewana na kila mmoja katika jamii na mwisho kuwaunganisha wanajamii. Haya ni maoni ya wahojiwa wetu ambao ni walimu kuhusu lugha ya Sheng na ikadhihirika wazi kuwa wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng. Vile vile kwa upande wa mielekeo ya wazungumzaji kuweza kuathiri uteuzi na matumizi ya lugha fulani na mzungumzaji, washiri wote sita wanasema ndio na kutoa sababu kuwa iwapo una mwelekeo ulio hasi kuhusu lugha fulani basi hutaweza kuitumia katika muktadha wowote ule.

Pia imedhihirika wazi kutokana na maoni ya walimu kuhusiana na swali la kumi na nane kuwa mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mwalimu. Walimu ambao wamejaza hojaji wameunga kauli hii mkono kwa maana wao kama walimu wa lugha wanapigia debe lugha ya Kiswahili sanifu ambayo inasahaulika na wanafunzi wengi ambao wameichangamkia lugha ya Sheng. Kulingana na maoni ya walimu, wanafunzi wameathirika sana na lugha ya Sheng na hivyo wanaogopa kuwa na uhusiano wa karibu na walimu hawa ambao wangewakemea iwapo wangetumia lugha ya Sheng wanapokuwa nao hadharani. Hili limesababisha kuwa na ufa kwa uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi.

Kwa kuzingatia swali la kumi na tisa, wahojiwa wetu ambao ni walimu wametoa maoni yao kuwa, hata iwapo Sheng ni lugha haina kanuni ambazo zinaiongoza katika matumizi yake na hivyo basi kukosa mpangilio maalum ambao huitambulisha lugha. Vile vile wameelezea kuwa kwa kuwa Sheng haina utamaduni unaoiongoza na hivyo basi haina mashiko yoyote katika jamii. Wanaongezeakwa kusema kuwa Sheng imeathiri matokeo ya mitihani hasa mtihani wa Kiswahili ambao ni wa muhimu sana kwa maisha ya mwanafunzi ili aweze kuhitimu na hivyo basi kile kinacho haribu kitu kingine kilicho muhimu basi hakina umuhimu wowote. Hivyo basi kusema kuwa Sheng isipewe nafasi yoyote shuleniili kuhifadhi lugha sanifu ya Kiswahili.

Kutokana na maoni haya ya walimu ni dhahiri kuwa walimu wako na mielekeo hasi kuhusu Sheng kama lugha. Hata ingawa wanaitambua Sheng kama lugha, ni wazi kuwa hawaiungi mkono kwani kwao, Sheng inathiri matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule. Katika mahojiano ya moja kwa moja hata hivyo, wanaunga mkono kuwa wanafunzi wanamielekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng kwani mara kwa mara wanawasikia wakizungumza lugha hiyo ukilinganisha na Kiswahili sanifu ambayo inazungumzwa kwa nadra sana.

3.2.3. Wafanyikazi wasio walimu

Katika sehemu hii, tumeweza kuwashirikisha jumla ya wafanyikazi wasio walimu kumi; watano wa kike na watano wa kiume. Upande wa umri ingawa wengine hawakuwa radhi kusema lakini tumepata kujua kuwa ni wa kati ya umri wa miaka ishirini na sita hadi hamsini na tano. Muda ambao wamefanya kazi shuleni humo ni kati ya miezi minne na miaka thelatini. Washiriki watano wamefika vyuo vya ufundi nawatano na wakifika katika shule za upili. Waliokuwa wamefika katika vyuo vya ufundi ndio wasimamizi katika maofisi

mbalimbali na wale ambao wamefika katika shule ya upili wengi wao nimabawabu na wapishi.

Makazi ya wengi wa wafanyikazi hawa ni mitaa kama vile Githurai, Mathare na pia Kibera ambapo lugha ya Sheng tuliyokuwa tunatafitia imemea mizizi. Kwa upande wa lugha wanazozifahamu vile vile imedhihirika kuwa wana hali ya utatulugha kwani kila mmoja ametaja lugha yake ya kienyeji, Kiswahili na Kiingereza. Washiriki wote kumi wameweza kuifahamu lugha inayowazaa na hutumia kwa mawasiliano yao na wenzao wanaoifahamu lugha hiyo.

Swali la nane linalouliza iwapo Sheng ni lugha, washiriki watano walitoa maoni yao kuwa Sheng sio lugha na kuitambua kama maneno ya vijana. Hata hivyo washiriki watano kati yao hasa mabawabu na wapishi wanakubali kuwa wao hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku mwiongoni mwao wenyewe na pia na wanafunzi ambao huwazungumzia kwa lugha hiyo ya Sheng. Swali iwapo wao hutumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni imejibiwa ndio na kutoa sababu kuwa ni njia rahisi ya kuwasiliana na wenzao hasa mabawabu na pia wapishi. Vile vile wanaelezea kuwa wanafunzi wanapenda kutumia lugha hii ya Sheng wanapozungumza kila mara na inawabidi pia kuitumia lugha hiyo ili waweze kuwasiliana na kuwa na uhusiano mzuri na wao.

Pia wanaongezea kuwa, wanapendelea lugha ya Sheng ingawa bado kwao hawakuiona kama lugha bali mambo ya vijana huku wakitoa sababu kuwa ni rahisi kutumia na pia kuelewa. Haya yametolewakama maoni ya kujibu swali la kumi ambalo lilitaka kujua iwapo mhusika anapendelea lugha ya Sheng au Kiswahili sanifu. Kulingana na wao, mielekeo ya wazungumzaji wa lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu kwani uzoefu wa kutumia lugha ya Sheng husababisha mhusika kusahau kaida ya lugha na kutumia maneno kwa muundo usiofaa au kwa kuvunjavunja muundo wa maneno hayo kwa kuyatamka au kuyaandika visivyo.

Kwa upande wa jinsia, wafanyikazi wasio walimu wanatoa maoni yao kuwa watu wa jinsia zote hutumia lugha ya Sheng. Wanafunzi kutoka shule zingine wanapokuja shuleni humo kwa ajili ya shughuli za michezo au tamasha mbalimbali kama za muziki husikika wakizungumza na kuwasiliana na wenzao wasichana kwa wavulana kwa kutumia lugha ya Sheng. Baadhi yao pia wanaelezea katika mahojiano ya moja kwa moja kuwa, wanapoelekea nyumbani wakati wa jioni na kuja kazini asubuhi, wao hukutana na wanafunzi kutoka shule tofauti za kutwa ambao hutumia lugha ya Sheng wasichana kwa wavulana.

Kutoathiriwa na lugha ya Sheng iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumika ni kauli ambayo washiriki wanane wanaikataa kwani wengi wao wameathiriwa na lugha ya Sheng kutokana na mzingira ambamo wao wanaishi katika mitaa mbalimbali katika jiji kuu la Nairobi. Wametoa sababu zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo kuhusu lugha moja hasa lugha ya Sheng au chanya au hasi. Wanasema kuwa ni kwa sababu ya kasumba ambazo wanazo hasa wanaume na pia wanawake kuziangazia lugha zingine kama zile za hadhi ya chini na za watu ambao hawajasoma huku wakirejelea lugha ya Sheng. Pia kulingana na maoni yao lugha kama ya Sheng huwa ya watu wahuni na pia wajanja ambao hawawezi kuaminika katika mambo au shughuli mbalimbali.

Kulingana nao, mielekeo ya wazungumzaji huathiri pakubwa uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji. Sababu zao zikiwa, mtu huchagua lugha anayoipenda na kuienzi kama iliyo bora zaidi na kuitumia katika mawasiliano. Katika mahojiano ya moja kwa moja, wengi wao wanakiri kwamba wao hujikakamua kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza na wakubwa wao kazini ili waonekane kuwa wao pia wamesoma na kuchukulia kama lugha ya heshima ukilinganisha na lugha ya Sheng. Kama ilivyo katika swali la kumi na sita, wameweza kukiri kuwa wanapotumia lugha ya Sheng katika mazungumzo yao na wanafunzi, kuna uhusiano mwema zaidi na wanafunzi hao ukilinganisha na labda wengine ambao hawatumia lugha ya Sheng wanapowasiliana na wao. Kulingana na wao wanafunzi wengi walimpenda yule aliyewasiliana na wao kwa kutumia lugha ya Sheng na kuwa marafiki zaidi ikilinganishwa na wafanyikazi wengine wanaotumia Kiswahili sanifu au Kiingereza katika mawasiliano yao na wanafunzi hao.

Jibu kuhusu iwapo mazingira wanamoishi mnachangia katika mielekeo yao kuhusiana na lugha ya Sheng wametoa kuwa ndio. Wameweza kutaja kuwa mazingira wanamoishi humu jijini ndiyo inayowafanya kujua lugha ya Sheng kwani wengi wao waliungama kuwa kabla waje jijini hawakuwa wanaifahamu lugha hii ya Sheng. Mielekeo juu ya lugha ya Sheng huweza kuathiri uhusiano baina yao na wanafunzi kwani wanafunzi huwachukulia wale ambao hawajui lugha ya Sheng kama watu ambao hawajui mengi, (... *hawajachanuka*). Waliongezea kuwa wanafunzi hawakuwapenda walimu ambao hawajui lugha ya Sheng na kutoa madai kuwa wao ni (...*washamba*) kwa maana hawajui lugha ya Sheng na wale wanaoifahamu na hata mara nyingine kuzungumza nao kuaminika kuwa ni (...*wajijini*) au (...*mtaani*).

Swali la kumi na tisa kuhusiana na nafasi ya lugha ya Sheng kwa kuzingatia katiba ambayo inampa Mkenya uhuru wa kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea limewachanganya wengi ambao imetubidi kuwafafanulia na kuwa na mahojiano ya moja kwa moja baada ya hojaji kurejeshwa huku swali hilo hawakuwa wamelijaza. Baada ya maelezo yetuna washiriki wetu kuelewa, wametoa maoni yao kuwa Sheng haistahili kukubaliwa kutumika katika mawasiliano rasmi kwani kulingana na wao, Sheng inawafanya vijana au watu kwa jumla kuwa wajanja. Waliongezea kuwa Sheng ibaki tu kule mitaani na kutumiwa na vijana wa mitaani bali isiruhusiwe kutumika katika miktadha rasmi kama ya shuleni.

Hivyo basi, kutokana na maoni ya wafanyikazi wasio walimu inadhihirika wazi kuwa wao pia wana mielekeo hasi kuhusiana na lugha hii ya Sheng ambayo wanaihusisha na watu wahuni na wajanja ambao wanapatikana katika vitongoji duni katika jiji kuu la Nairobi. Pia kwao wanaiona Sheng kama mambo ya vijana bali hawaitambui kama lugha.

3.2.4. Wazazi

Wazazi ambao tumewalengakwa ajili ya utafiti huu ni wazazi wa wanafunzi wanaosomea katika shule ya upili ya Jamhuri. Wakati shule zinapofunguliwa wazazi wengi humiminika shuleni humo kwa ajili ya kulipa karo na hata kuwaleta wana wao shuleni na basi hii ilikuwa wakati mwafaka kwa sisi pia kuzuru shuleni humo na kuweza kuwapa hojaji zetu ili waweze kutupa maoni yao kulingana na maswali ambayo tumewaandalia kuhusiana na utafiti wetu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu Sheng; kwa kurejelea shule ya upili ya Jamhuri, ipatikanayo jijini Nairobi.

Kwa umri, wazazi ambao tumewahoji ni kati ya miaka arubaini hadi miaka sabini. Wanawake wameonekana kuwa kati ya miaka arubaini hadi hamsini ilhali wanaume wengi umri wao ni kati ya miaka hamsini hadi sabini. Tumezingatia pia jinsia kwa usawa kwa kuwapa hojaji tano wanawake na hojaji tano wanaume. Kwa upande wa elimu, tumepata kuwa washiriki watano wamesoma hadi chuo cha ufundi, watatu kusoma hadi shule ya upili nao wawili wamefika katika shule ya msingi.

Washiriki sitaambao wameshirikishwa katika kujibu maswali ya hojaji zetu ni wazazi wa wanafunzi katika vidato vya chini (kidato cha kwanza na pili) nao wannewakiwa ni wazazi wa wanafunzi katika vidato vya juu (kidato cha tatu na nne). Hivyo basi, wengi wao wamekuwa wazazi wa wanafunzi wa shule hii kati ya mwaka mmoja na miwili. Kwa upande wa makazi nao, wazazi wote kumi wa wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri wanaishi katika mitaa au vitongoji vya jiji kuu la Nairobi ambako lugha ya Sheng hutumika sana.

Maeneo haya ni kama vile, Mathare, Githurai, Babadogo, Kibera na hata Kangemi. Wengi wa wazazi hawa pia walikuwa ni wa uwililugha kwani katika swali kuhusu lugha wanazozifahamu, kila mmoja ametaja lugha yake ya kienyeji kisha Kiswahili isipokuwa washiriki wawili tu waliotaja pia Kiingereza na kuonyesha kuwa walikuwa na utatulugha.

Kila mhusika ameweza kuitaja lugha iliyomzaa na kumlea na kuongezea kuwa huwa wanaitumia katika mawasiliano yao mara kwa mara wakiwa pamoja na wenzao wanaoifahamu hiyo lugha. Swali la iwapo Sheng ni lugha limekubaliwa na washiriki wanane tuliowahoji ambao ni wazazi isipokuwa tu washiriki wawili ambao walisema hawaijui kama Sheng ni lugha au la. Washiriki wananeambao wamekubali kuwa Sheng ni lugha wamesema kuwa wao huitumia lugha hiyo ya Sheng wakati wakiwa nyumbani na watoto wao, katika makazi yao na sokoni wakiwa na marafiki wenzao kwa mawasiliano. Wametaja Sheng kuwa ni rahisi kutumia na kuwa ni rahisi kuelewa kwani msamiati wake ni mwepesi na pia haina sheria za kisarufi ambazo zatakiwa kuangaziwa.

Wazazi wote kumi tuliowahoji walikubali kuwa wao hutumia lugha ya Sheng wakiwa na watoto wao nyumbani na hata mara nyingine wakikutana na wanafunzi wengine kutoka shule hii wakienda shuleni au wakirudi nyumbani. Sababu ambazo wamezitoa katika kauli hii ni kuwa watoto wao hupenda kutumia lugha hii ya Sheng wakiwa nyumbani na basi kuwalazimu wazazi wao pia kutumia lugha hiyo wanapowasiliana au kuzungumza na wao. Pia kulingana na baadhi yao wamesema kuwa lugha ya Sheng ni rahisi kuzungumza na kuelewa ukilinganisha na Kiingereza au Kiswahili sanifu na hivyo basi wanapendelea lugha ya Sheng zaidi kuliko lugha ya Kiswahili sanifu kwani ndiyo lugha wanayoitumia kwa wingi sana katika mawasiliano yao ya kila siku.

Wahojiwa wetu wote wamekubaliana na kauli kuwa mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu kwani wazungumzaji wa lugha ya Sheng hawakuweza kuzungumza Kiswahili sanifu wakati wanafaa kuzungumza katika miktadha rasmi. Hivyo basi upendeleo wao kwa lugha ya Sheng umesababisha uzungumzaji wa Kiswahili kibovu na hata wakati mwingine wengine kushindwa kutumia Kiswahili kabisa.

Kwa kurejelea suala la jinsia, wahojiwa wetu wametoa kauli zao kuwa jinsia zote zinapendelea kutumia lugha ya Sheng kwa usawa. Sababu zao zikiwa kuwa, wao wana watoto wa hizi jinsia mbili na huwa wanawaona na kuwasikia mara kwa mara wakiwasiliana

kwa kutumia lugha ya Sheng. Wao pia huwasiliana miongoni mwao (wa kiume na wa kike) na hivyo basi jinsia zote hutumia lugha ya Sheng kwa usawa.

Kuhusu hoja ya kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo mtu anaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumika ni kauli ambayo ilikataliwa na kila mhojiwa wetu ambao ni wazazi. Kwa maoni yao wanasema kuwa watu wengi huathirika na lugha ya Sheng kutokana na mazingira ambamo lugha hiyo inatumika. Hii ni kwa sababu mawasiliano yote katika mitaa hii ni ya lugha ya Sheng na hivyo inambidi mtu kujua lugha hiyo ya Sheng ili kuweza kuwa na mwingiliano mwema na watu wengine katika mazingira hayo.

Sababu zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo kuhusu lugha ya Sheng hasa mwelekeo chanya ni urahisi wa kutumia na kuelewa lugha hii bila ya kuwa na kaida na sheria nyingi funge kama ilivyo lugha ya Sheng. Haya ni maoni ya wahojiwa ambao wana mwelekeo chanya kuhusiana na lugha ya Sheng. Sababu nyingine wanayoitoa ya kuwafanya kuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng ni kuwa watu wengi wanaitumia na hivyo basi kuwaunganisha watu wengi kutoka makabila mbalimbali. Umoja unaoletwa na kupatikana miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Sheng ndio unaowafanya watu wetu wengi kuipendelea katika mawasiliano na mazungumzo yao ya kila siku.

Mielekeo ya wazungumzaji kuweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji imekubaliwa na wazazi ambao wamejaza hojaji ambazo tumewaandalia na kuwapa. Sababu zao zikiwa, lugha ambayo mzungumzaji haipendi hataweza kuitumia katika mazungumzo au mawasiliano yake ya kila siku. Hivyo basi mwelekeo wa mzungumzaji kuhusiana na lugha fulani huathiri uteuzi na utimizi wa lugha husika. Vile vile, wamekiri kuwa matumizi ya lugha ya Sheng yameweza kuathiri utendakazi wa watoto wao shuleni hasa katika somo la Kiswahili. Sio watoto wao pekee bali pia wanasema kuwa watoto wa majirani wao imegunduliwa kuwa wameathirika sana katika masomo yao hasa katika somo la Kiswahili kutokana na athari ya lugha ya Sheng ambayo wanaitumia katika mazungumzo na mawasiliano yao ya kila siku. Mazingira pia ambamo mhusika anaishi huchangia katika mwelekeo wake kuhusiana na lugha ya Sheng. Sababu inayotolewa ni kuwa inambidi mzungumzaji kuchangamkia lugha ambayo inatumika kwa wingi katika eneo analoishi ili kuweza kuwasiliana na wenzake na hivyo basi mazingira huathiri pakubwa kwa mwelekeo wa mzungumzaji wa lugha ya Sheng.

Mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mzazi kwani kuna maneno na msamiati ambao hutumiwa na wazazi kushindwa kuelewa na hata kwa wakati mmoja kudhani kuwa labda wanawasengenya na hivyo basi kuleta ugomvi au hali ya utata baina yao. Baada ya mzazi kugundua kuwa lugha ya Sheng ndio inayomfanya mtoto wake kutofanya vyema katika masomo mengine hasa somo la Kiswahili, huwa wanaanza kupewa vikwazo vya kutotumia lugha ya Sheng katika mazungumzo yao kila wakati ili kujaribu kupata mazoezi ya ziada ya lugha ya Kiswahili.

Ingawa wazazi walitumia hii lugha ya Sheng pia na katiba iliweza kukubalia Wakenya kuchagua na kutumia lugha na utamaduni wanaoupendelea, kwa kurejelea lugha ya Sheng, wanatoa maoni yao kuwa lugha ya Sheng isiweze kukubaliwa kama lugha ya kutumiwa katika miktadha rasmi kwani wao pia wanaichukulia lugha ya Sheng kama lugha ya mtaani au nyumbani.

Kutokana na maoni ya wazazi ambao wamehojiwa, wameonekana kutokuwa na shida kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi / watoto wao katika mawasiliano yao na mazungumzo yao ya kila siku lakini bado wanahimiza kuwa ibaki kuwa tu lugha ya mtaani au nyumbani na wala isiweze kukubaliwa kutumiwa katika shughuli au miktadha rasmi. Kwa jumla wazazi hawa pia wana mielekeo chanya kuhusiana na lugha ya Sheng.

3.3. Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa mielekeo ya wazungumzaji wa lugha fulani huwafanya kuweza kuipenda lugha hiyo na kuitumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Kwa mfano wanafunzi katika mkutadha wa utafiti huu wameonekana wazi kuwa na mielekeo chanya kuhusiana na Sheng. Vile vile, sababu za kuipenda lugha hii zimeweza kutolewa na watafitiwa wote.

Ingawa mazingira na hata marika huweza kuwa na athari kuhusiana na kujua na kutumia lugha yoyote ile, tumeweza pia kufahamu kuwa mielekeo ya wahusika au wazungumzaji huweza kuathiri pakubwa ufahamu na utumizi wa lugha fulani. Hili ni dhahiri kwani baadhi ya walimu, wafanyikazi wasio walimu na hata baadhi ya wazazi ambao pia wanaishi katika mitaa ambamo lugha ya Sheng imesheheni na kutumiwa kwa wingi hawatumii lugha ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku. Wao, kinyume na wanafunzi, wameonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng. Baadhi ya walimu na wazazi wametoa maoni yao kuwa Sheng huchangia pakubwa katika matokeo duni ya somo la Kiswahili na hata masomo mengine kwa kiasi fulani.

Vile vile baadhi ya walimu na wazazi wamechukulia lugha ya Sheng kama lugha ya watu wahuni na ndio maana wakawa na mielekeo hasi kuhusiana na lugha hii ya Sheng. Kando na hayo, wazazi pia walizidi kutoa maoni kuwa, baadhi ya wana wao hawazifahamu mila na tamaduni za lugha zao za kienyeji kutokana na madhara ya lugha ya Sheng kwa kutaja kuwa mwacha mila ni mtumwa katika mahojiano ya moja kwa moja ambayo tumekuwa nayo na baadhi yao.

Jambo jingine muhimu ni kuwa wakazi wa jiji la Nairobi na hasa katika mitaa mingi ambamo lugha ya Sheng inatumiwa ni kutoka makabila mbalimbali. Kila mmoja alijaza hojaji zetu katika swali la saba ameweza kuitaja lugha iliyomzaa na kumlea ambazo ni tofauti tofauti ndio maana tukajua kuwa watu wa makabila tofauti wanaishi katika mitaa moja humu jijini na wana wao ambao wameipenda na kuchangamkia lugha ya Sheng kwa sana. Hii inamaanisha kuwa lugha ya Sheng haitumiwi na watu kutoka tu kabila moja bali imeweza kukolea na kutumiwa na watu kutoka makabila mbalimbali.

Hivyo basi, ni dhahiri kuwa mielekeo ya wazungumzaji iwe aidha chanya au hasi kuhusu lugha fulani na katika muktadha huu ukiwa ni lugha ya Sheng, hutegemea kupenda kwa mtu lugha fulani na pia athari ya marika katika kiwango fulani. Hii ndio sababu wanafunzi wengi wameonekana kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng ukilinganisha na wahusika wengine ambao kwa kiasi fulani wameonekana kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA MJADALA KUHUSU MATOKEO YA UTAFITI

4.1. Utangulizi

Sura hii ya nne inaangazia mjadala unaozuka kutokana na utafiti huu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusu Sheng katika shule za sekondari; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, ipatikanayo jijini Nairobi kwa kujadili matokeo/majibu ambayo tumepata kutokana na hojaji ambazo tumeweza kuwashirikisha wanafunzi arobaini (kumi kutoka kila kidato), walimu sita wa lugha tukizingatia jinsia zote kwa usawa, wafanyikazi wasio walimu kumi wa jinsia zote kwa usawana wazazi kumi pia wa jinsia zote kwa usawa wa shule ya upili ya Jamhuri. Mjadala huu umetupa mwanga nakutuwezesha kujua mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari.

4.2.Uchanganuzi wa Matokeo ya Utafiti kuhusu Mielekeo ya Wanafunzi na Wadau kuhusu Sheng

Mjadala wetu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusu Sheng unajadiliwa kwa kuelekezwa na malengo ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu tunataka kujua iwapo matokeo ya utafiti huu yameweza kuwiana na malengo yetu ya utafiti na pia kujibu maswali ya utafiti huu. Hivyo basi, mjadala wetu unaelekezwa na malengo ya utafiti huu na hivyo basi kuangaziwa kwa sehemu nne kama yalivyo malengo yetu.

4.2.1. Kubaini iwapo Wanafunzi na Wadau wengine wanaenzi Lugha ya Sheng kuliko Lugha zingine wanazozifahamu

Kutokana na utafiti wetu na hojaji ambazo tumewapa wahojiwa wetu, tumepata kuwa kati ya wanafunzi arubaini ambao tumewahoji, wote wameonekana kuenzi lugha ya Sheng kutokana na namna ambavyo wameweza kuyajibu maswali yetu. Hii ilijumuisha washiriki arubaini ya wanafunzi ambao imeonekana kuenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu.

Swali kuhusu lugha wanazozifahamu, baadhi yao wametaja lugha ya Sheng kama moja wapo ya lugha wanazozifahamu. Hili ni dhahirisho tosha kuwa wana mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng. Kwa hivyo jumla ya wahojiwa wetu wanafunzi, ambao ni arubaini, wote wameonekana kupenda lugha ya Sheng katika mawasiliano yao hata wakiwa shuleni. Hii niasilimia sabini (70%) ya jumla ya washiriki walio hojiwa. Kati ya walimu sita waliohojiwa, ni mwalimu mmoja tu ametoa maoni yanayoashiria kuwa anaipenda lugha ya Sheng na


kuitumia katika mawasiliano ya mara kwa mara hasa akiwa nyumbani .Makazi yake pia ni katika mitaa ya jijini Nairobi (Githurai) ambako watu wengi wanaitumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku.Hii inajumuisha asilimia mbili (02%) ya walimu wanaoenzi lugha ya Sheng. Wafanyikazi wasio walimu wanane kati ya kumi katika shule ya upili ya Jamhuri wanaonekana kuenzi lugha ya Sheng kutokana na namna ambavyo wameyajibu maswali katika hojaji. Hii imewakilisha asilimia kumi nanne (14%) ya wafanyikazi wasio walimu wanaoonekana kuenzi lugha ya Sheng. Wazazi wanane kati ya wazazi kumi ambao tumewahoji na kuwapa hojaji kujaza wameonekana kuenzi lugha ya Sheng ambayo ni sawa na asilimia kumi na nne (14%). Tumeweza kuweka data hiikwa muhtasari kama ilivyo katika jedwali: 4.1;

Jedwali: 4.1; Watafitiwa wanaoenzi Lugha ya Sheng kuliko Lugha zingine wanazozifahamu

Washiriki	Wanaoenzi lugha ya Sheng	Asilimia
Wanafunzi	40	70%
Walimu	01	02%
Wafanyikazi wasio walimu	08	14%
Wazazi	08	14%
Jumla	57	100%

Data hii tumeweza kuiwekwa katika muhtasari katika pai chati kama ilivyo katika chati 4.1 hapa chini;

Chati: 4.1. Watafitiwa wanaoenzi Lugha ya Sheng kuliko Lugha zingine wanazozifahamu




Hata hivyo, kuna wahojiwa wetu ambao tumewahojina kuwapa hojaji kujaza na kugundua kuwahawaenzi lugha ya Sheng. Kati ya wanafunzi arubaini, hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyetoa maoni kuwa haienzi lugha ya Sheng. Hii ikatupa asilimia sufuri (00%) ya wanafunzi wasioenzi lugha ya Sheng. Kati ya walimu sita walioshirikishwa katika utafiti huu, tano kati yao walitoa maoni ya kuashiria kutoenzi lugha ya Sheng. Hii ilitupa asilimia hamsini na sita (56%). Wafanyikazi wasio walimu na wazazi wa wanafunzi katika shule ya upili ya Jamhuri wawili wawili mtawalia walitoa maoni yaliyoashiria kutoenzi lugha ya Sheng. Hii ilitupa asilimia ishirini na mbili (22%) kwa kila mshirika, (wafanyikazi wasio walimu na wazazi), kama ilivyo katika muhtasari katika jedwali 4.2;

Jedwali: 4.2; Watafitiwa wasioenzi Lugha ya Sheng

Washiriki	Wasioenzi lugha ya Sheng	Asilimia
Wanafunzi	00	00%
Walimu	05	56%
Wafanyikazi wasio walimu	02	22%
Wazazi	02	22%
Jumla	09	100%

Tumeweza kuiweka data hii katika pai chati 4.2, hapa chini ilikuonyesha idadi kwa asilimia ya wahojiwa ambao hawaienzi lugha ya Sheng.

Chati: 4.2. Watafitiwa wasioenzi Lugha ya Sheng



Tanbihi: Kutokana na pai chati 4.2, kuhusu washiriki wasioenzi lugha ya Sheng, tunaona kuwa hamna mwanafunzi hata mmoja asiyeenzi lugha ya Sheng na ndio sababu asilimia yake ni sufuri (0%). Hili ni dhihirisho tosha kuwa wanafunzi washiriki wote arubaini wanaenzi lugha ya Sheng kama ilivyoonyeshwa katika chati 4.1 hapo juu.

4.2.2. Miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia lugha Sheng

Kwa kuzingatia miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia lugha ya Sheng, baadhi ya maswali katika hojaji zetu yalilenga kujibu swali hili ambalo ni mojawapo ya malengo ambayo tumekuwa tunahitaji kutimiza katika utafiti huu wetu.

Wanafunzi wameonekana kutumia lugha hii ya Sheng karibu katika shughuli zao zote hasa katika mawasiliano yao ya kila siku. Wameonekana kutumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni katika mazungumzo yao na wenzao kwa kiasi fulani na pia kwa sana wakiwa nyumbani au makazi yao. Katikaidadi ya wanafunzi arubaini ambao tumewahoji na kujaza hojaji ambazo tumewapa, wanafunzi arubaini wote walionekana kuichangamkia lugha hii ya Sheng katika

mawasiliano yao yote ya nyumbani huku takribani wanafunzi thelathini kati ya arubaini waliojaza hojaji kusema kuwa wao hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao wakiwa shuleni. Kati ya walimu sita ambao wameshirikishwa katika kujaza hojaji zetu, wote sita wameonekana kutumia lugha ya Sheng katika shughuli zao za nyumbani huku mmoja tu akisema kuwa yeye hutumia lugha ya Sheng akiwa shuleni hasa akiwa uwanjanai na wanafunzi wakishiriki michezo. Hii ni kwa sababu hushiriki michezo na wanafunzi kila siku uwanjani wakati wa michezo.

Kati ya wafanyikazi wasio walimu kumi ambao tumewashirikisha katika mahojiano yetu na kujaza hojaji, watano walikubali kuwa wanatumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni na kutoa sababu zao kuwa wanajipata tu wakitumia kwani baadhi ya wanafunzi huwazungumzia katika lugha hii ya Sheng. Baadhi yao ni mabawabu na wapishi wa shule hii. Lakini katika muktadha wa nyumbani, wote kumi walionekana kutumia lugha hii katika mawasiliano yao ya kila siku na familia zao pamoja na wakazi wenzao wanakoishi.


Wazazi nao walionekana kuchangamkia lugha ya Sheng kwa sana wakiwa nyumbani. Katika hojaji zetu, wazazi kumi wote walionekana kuitumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku wakiwa nyumbani. Kati ya hao kumi, ni wawili tu ambao waliongezea kuwa pia wanaitumia lugha hiyo ya Sheng wakiwa shuleni hasa wakati ambao wametembelea shule kwa ajili ya kulipa karo au kujua hali ya masomo ya wana wao. Waliweza kuzungumza Sheng na mabawabu na baadhi ya wapishi ambao wanakutana nao kule shuleni. Kuna miktadha mingi ambamo Sheng hutumika lakini tumeangazia miktadha miwili tu ambayo ni shuleni na nyumbani. Tumeweza kupangilia habari hii kwa muhtasari kama ilivyo katika jedwali: 4.3;

Jedwali: 4.3; Miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia Lugha Sheng

Washiriki	Muktadha wa shuleni	Muktadha wa nyumbani
Wanafunzi	30	40
Walimu	01	06
Wafanyikazi wasio walimu	05	10
Wazazi	02	10
Jumla	38	66

Kutokana na data hii, tunaona kuwa lugha ya Sheng inatumiwa kwa wingi katika muktadha wa nyumbani ukilinganishwa na muktadha wa shuleni. Hii ni kutokana na idadi ya jumla ya washiriki sitini na sita ambao wote walionekana kutumia lugha ya Sheng katika muktadha wa nyumbani huku washiriki thelathini na nane kuonekana kuitumia lugha ya Sheng katika muktadha wa shuleni. Hivyo basi ni wazi kuwa lugha ya Sheng hutumiwa kwa sana katika mazingira na miktadha ya nyumbani katika shughuli za mawasiliano. Ujumbe huu tumeweza kuuweka katika muhtasari katika grafu: 4.1;

Grafu: 4.1; Miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia Lugha Sheng



4.2.3. Mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya Lugha ya Sheng na wanafunzi

Mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi imeangaziwa katika hojaji zetu na kupata maoni mbalimbali ya wazazi na walimu. Kati ya wazazi kumi ambao tuliwahoji na kujaza hojaji zetu, ni wazazi wawili pekee ambao walionekana kuwa na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi. Wanane kati yao walionekana kuwa na mielekeo hasi na kutoa sababu zao kuwa hii imesababisha kuwepo kwa matokeo duni miongoni mwa wanafunzi na pia kuwaingiza katika makundi ya wahuni. Waliongezea kuwa tabia za watoto wao zimezorota kutokana

namatumizi ya lugha hii ya Sheng ambayo imewashirikisha na makundi ya vijana walaghai na wapotovu wa nidhamu.


Walimu nao walionekana kuwa na mitazamo na mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi. Sababu ilikuwa kwamba, wanafunzi hawa wamezoea kutumia Sheng jambo ambalo limeathiri matumizi ya Kiswahili sanifu na hivyo basi kuwa na matatizo ya matamshi na pia maandishi katika mazungumzo na kuandika mtawalia. Katika mitihani yao, kumekuwa na makosa mengi ya hijai hasa katika insha zao ambapo athari ya lugha ya Sheng imejitokeza wazi wazi. Walimu wote sita ambao tuliwapa hojaji walionekana kuwa na mitazamo na mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi. Tumeweza kuweka habari hii kwa muhtasari katika jedwali: 4.4;

Jedwali: 4.4; Mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi

Washiriki	Mitazamo na mielekeo chanya	Mitazamo na mielekeo hasi
Wazazi	2	8
Walimu	0	6
Jumla	2	14

Jedwali 4.4, linalotoa muhtasari wa mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi, na ni wazi kuwa wazazi na walimuwengi wana mitazamo na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng inavyotumiwa na wanafunzi. Matokeo haya yameweza kujibu swali la kutathmini mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu wa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi wa shule hii ambalo lilikuwa miongoni mwa malengo yetu katika utafiti huu. Hakuna mwalimu hata mmoja ambaye amekuwa na mitazamo na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi huku wazazi wawili pekee wakiwa na mitazamo na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi. Kando na hayo, wazazi wanane wameonekana kuwa na mitazamo na mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi huku walimu sita pia wakiwa na mielekeo sawia. Hii ilitupa jumla ya washiriki (wazazi na walimu) kumi na wane ambao wana mitazamo na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng. Tumeweza kuweka ujumbe huu kwa muhtasari katika grafu: 4.2;

Grafu: 4.2; Mitazamo na mielekeo ya wazazi na walimu kuhusu matumizi ya Lugha ya Sheng na wanafunzi



Tanbihi: Grafu hii inaonyesha idadi ya wale waliokuwa na mielekeo ama chanya au hasi baina ya walimu na wazazi wa wanafunzi wa shule ya upili ya Jamhuri. Kutokana na grafu hii, ni dhahiri kuwa, hakuna mwalimu hata mmoja kati ya sita walioshiriki kujaza hojaji katika utafiti huu alikuwa na mwelekeo chanya kuhusiana na lugha ya Sheng.

4.2.4. Mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi

Hojaji zetu pia ziliandaliwa kwa kushirikisha maswali ambayo yamenuia kujibu swali la kutaka kujua mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Kutokana na majibu ambayo tulipata kutoka katika hojaji zetu, tumepata kujua kuwa wafanyikazi wasio walimu huchangia pakubwa kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

Kuna maswali kadhaa ambayo yalilenga kujibu swali hili ambalo pia ni kati ya malengo ya utafiti huu wetu. Kutokana na majibu ambayo tumepata kutoka kwa wahojiwa wetu ambao

ni wafanyikazi wasio walimu, tumegundua kuwa wafanyikazi hawa wamechangia pakubwa katika matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

Kwa kujibu swali la iwapo wao hutumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni, wafanyikazi watano kati ya kumi walikiri kuwa wao hutumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni katika mawasiliano yao na wanafunzi. Hawa walishirikisha mabawabu na wapishi ambao wanatagusana na wanafunzi katika shughuli za kila siku. Kuangazia swali la iwapo wao huenzi lugha ya Sheng, wafanyikazi wasio walimu wanane walikubali katika hojaji zetu kuwa wao huenzi lugha ya Sheng na hivyo basi kutokana na mtagusano wao wa kila siku na wanafunzi, basi wamekuwa na mchango mkubwa kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

Kati ya wahojiwa wetu kumi ambao walijaza hojaji, watano walionekana kuitumia lugha ya Sheng wakiwa shuleni pamoja na wanafunzi na hivyo basi kuwa na mchango mkubwa kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Pia wafanyikazi wasio walimu katika shule hii wapatao wanane kati ya kumi ambao walijaza hojaji zetu, wameonekana kuenzi lugha hii ya Sheng na kwa kuwa wamekuwa na mtagusano wa karibu na wa kila siku na wanafunzi hawa, basi wana mchango mkubwa kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

Jedwali: 4.5; Mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi


Wafanyikazi wanaotumia Lugha ya Sheng	Wafanyikazi wanaoenzi Lugha ya Sheng
5	8

Kama ilivyo katika jedwali 4.5, washiriki wetu ambao ni wafanyikazi wapatao watano walionekana kuwa na mchango kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi kwa kuitumia wakiwa shuleni. Hii inatupa asilimia thelathini na nane (38%) ya wafanyikazi wasio walimu katika kutoa mchango wao kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Wafanyikazi wanane nao kati ya kumi walionekana kuenzi lugha hii ya Sheng na baada ya kuwa na mahojiano ya moja kwa moja na pia baada ya kujaza hojaji zetu, walionekana kuenzi lugha ya Sheng na kukiri kuwa huwa wanaitumia

sana katika mawasiliano yao ya kila siku. Hii inatupa asilimia sitini na mbili (62%) ya wafanyikazi wasio walimu ambao wamekuwa na mchango kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi.

Tumeweza kuuwasilisha ujumbe huu kwa kutumia pai chati ambayo imetoa muhtasari wa mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi katika pai chati 4.3;

Chati: 4.3; Mchango wa wafanyikazi wasio walimu na wadau wengine kuhusu matumizi ya Lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi



4.3. Hitimisho

Mjadala wetu kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, jijini Nairobi umeweza kuongozwa na malengo yetu manne ambayo tulikuwa nayo katika utafiti huu. Malengo hayo yamekuwa ya kutuelekeza na kutupa mwanga kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari kuhusu lugha pendwa ya Sheng.

Kutokana na mjadala wetu, tumeweza kutambua kuwa malengo yetu yote yameweza kufanikishwa kutokana na majibu ambayo tumepata kutoka kwa washiriki wetu ambao

wamejaza hojaji mbalimbali ambazo tuliwaandalia na kuweza kuyajadili kwa kuongozwa na malengo yetu. Pia mahojiano ya moja kwa moja ambayo tulikuwa nayo na washiriki wetu katika utafiti huu yameweza kufanikisha matarajio yetu. Hivyo basi, tumepata kujua kuwa wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri wamekuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Sheng na hivyo kufanikisha utafiti wetu kwani malengo yetu yote na ambayo yamefanikisha utafiti huu yaliweza kuafikiwa. Hata hivyo baadhi ya walimu wa lugha ambao walijifanya kuwa wazee vijana waliichangamkia lugha ya Sheng lakini kwa uoga na kutotaka kujisaliti wakawa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1. Utangulizi

Katika sura hii tunaangazia muhtasari wa utafiti huu, mahitimisho yetu kuhusiana na utafiti huu na pia mapendekezo ambayo tumetoa ili yaweza kushughulikiwa na watafiti wengine wa baadaye.

5.2. Muhtasari

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti ambao ulituongoza kupata maswli yetu ya utafiti na malengo ambayo yalituelekeza katika kujua mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri kuhusu lugha ya Sheng. Tumeweza pia kutaja umuhimu wa utafiti huu kwani ungeweza kuwasaidia watunga sera ya lugha kuhusu nafasi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Tumeweza pia kuangaziayale yaliyoandikwa kuhusu lugha ya Sheng.

Ili kufanikisha haya, tumeweza kuongozwa na nadharia ya kisaikolojia ya jamii ambayo imetusaidia kujua mielekeo ya wahusika kuhusiana na lugha Sheng kama tulivyo shughulikia katika kazi yetu. Tumeweza kuchagua mbinu mwafaka za kufanyia utafiti huu na pia kuichagua shule ya upili ya Jamhuri kama mahali petu pa kufanyia utafiti baada ya kupata habari kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi wanaosomea katika shule hii walizaliwa na kukua na hata kuishi hadi sasa katika mitaa ya mjini Nairobi ambamo lugha ya Sheng inatumika kwa wingi sana.

Katika sura ya pili, tuliangazia mielekeo katika sera ya lugha nchini Kenya kufikia sasa kihistoria. Hili limeangaziwa katika sehemu mbalimbali kama vile; kuangazia mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya enzi ya ukoloni, mielekeo kuhusu lugha nchini Kenya baada ya ukoloni na pia kuangazia sera ya lugha nchini Kenya kwa mujibu wa katiba ya Kenya 2010. Haya yametusaidia pakubwa katika uelewa wa dhana ya mielekeo kuhusu lugha hasa lugha ya Sheng ambayo tumetafitia.

Katika sura ya tatu, tuliweza kuangazia matokeo ya utafiti huukwa kuangazia majibu yote ambayo tumeyapata kutokana na hojaji zetu ambazo tumewashirikisha wanafunzi, walimu, wafanyikazi wasio walimu na wazazi wa shule ya upili ya Jamhuri. Maoni ya washiriki wetu yameweza kuangaziwa na kutiliwa maanani jinsi yalivyotolewa na washiriki kwani

nimuhimu katika mjadala ambao umefanikisha utafiti huu kuhusiana na mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusiana na lugha ya Sheng.

Katika sura ya nne, tumeweza kujadili, huku tukiwa tunaongozwa na matokeo ya utafiti huu ambayo tumeyapata kutokana na hojaji ambazo washiriki wetu wameweza kujaza na pia kutokana na mahojiano yetu ya moja kwa moja na washiriki wetu. Mjadala huu uliweza kuongozwa na malengo ambayo tumetaka kujua iwapo yalikuwa yameafikiwa kutokana na matokeo au majibu ambayo tumepata kutoka kwa washiriki waliojaza hojaji na pia wale waliohojiwa moja kwa moja. Tumeweza kupata kuwa wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri wana mielekeo chanya kuhusiana na lugha ya Sheng. Wanafunzi na wadau wengine pia wana mielekeo ya kuenzi lugha ya Sheng. Kama moja wapo ya malengoya utafiti huu, tumeweza kupata ufahamu kuwa washiriki wengi walienzi lugha ya Sheng.

Pia imetambulika kuwa washiriki wengi wanatumia lugha ya Sheng katika miktadha ya nyumbani ikilinganisha na miktadha ya shuleni. Hili pia limeweza kufanikisha lengo letu la kutaka kujua miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine hutumia lugha ya Sheng. Nayo mitazamo ya walimu na wazazi kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng na wanafunzi iligundulika kuwa hasi kwani kwa pamoja waliiona lugha ya Sheng kama chanzo cha matokeo mabovu ya wanafunzi katika mitihani yao. Wafanyikazi wasio walimu na wazazi wameonekana kuwa na mchango mkubwa kuhusu matumizi ya lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu tumepata kujua kuwa wafanyikazi wasio walimu na wazazi wengi hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku na wanafunzi. Hii imesababishia wanafunzi kuichangamkia lugha hii ya Sheng hata katika mawasiliano yao ya kila siku wakiwa nyumbani na hata shuleni kwani walikuwa wazungumzaji wengine ambao wanazungumza nao kwa kutumia lugha hii ya Sheng.

5.3. Mahitimisho

Utafiti huu umekuwa unachunguza mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule za sekondari kuhusu Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, mjini Nairobi. Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa mielekeo chanya kuhusiana na lugha ya Sheng miongoni mwa wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri. Hii ni kutokana na maoni na habari ambayo tumepata kutoka kwa wahojiwa ambao tumewahoji na wale ambao wamejaza hojaji mbalimbali.

Tumegundua kuwa wanafunzi wengi wana mielekeo chanya kuhusu Sheng na hii ni kutokana na maeneo wanakoishi ambako Sheng hutumiwa kwa wingi sana jambo ambalo limesababishia wanafunzi hawa hata kuendeleza hali hii hadi shuleni katika mawasiliano yao ya kila siku. Hali hii pia imetokana na kutaka kuficha ujumbe kutoka kwa kundi fulani la watu. Walikozaliwa na kuishi hadi wa leo, wanafunzi hawa hutaka kuficha ujumbe kutoka kwa rika fulani ili wasiweza kuwaelewa hasa wanapozungumza kuhusu jambo fulani ambalo ni la siri wasilohitaji kundi lengine kuelewa hasa wazazi wao.

Malengo ya utafiti huu pia yameafikiwa vyema na matokeo ya utafiti. Lengo la kwanza lililenga kubaini iwapo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri wanaenzi lugha ya Sheng kuliko lugha zingine wanazozifahamu. Utafiti huu umebainisha kuwa wanafunzi na wadau wengine katika shule ya upili ya Jamhuri wanaenzi lugha ya Sheng na kuitumia katika mawasiliano yao ikilinganishwa na lugha zingine wanazozifahamu. Hii imedhihirika wazi pale ambapo hojaji ambazo zimejazwa zimeonyesha kuwa wahusika wote wanapendelea sana lugha ya Sheng na hata mara kwa mara katika mahojiano wamejipata wakiyajibu baadhi ya maswali ambayo tuliwauliza kwa kutumia lugha ya Sheng.

Lengo la pili lilikuwa kutambua miktadha ambamo wanafunzi na wadau wengine wa shule ya upili ya Jamhuri hutumia lugha ya Sheng katika shughuli zao za kimawasiliano. Lengo hili pia limeafikiwa vyema kwani wanafunzi na wadau wa shule ya upili ya Jamhuri wanatumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao. Tulipokuwa shuleni, tuliweza kuwasikia wanafunzi wakitumia lugha hii wanapowasiliana na hata wazazi tuliwapata wakiwa wamekuja kutembelea watoto wao shuleni, tuliweza kuwasikia wakiwasiliana kwa kutumia lugha ya Sheng. Wafanyikazi shuleni pia wamekuwa wanawasiliana wao kwa wao kwa kutumia lugha ya Sheng na pia tumewasikia wakiwasiliana na wanafunzi kwa lugha ya Sheng. Tunapowauliza mbona wanawasiliana na wanafunzi kwa lugha ya Sheng, wanatarifu kuwa wanafunzi wengi wanaenzi lugha ya Sheng na wakati mwingine wangekosa kuelewana iwapo hawangetumia lugha ya Sheng.

4.4. Mapendekezo

Utafiti huu umelenga kutathmini mielekeo ya wanafunzi na wadau wa shule za sekondari kuhusu Sheng; kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, mjini Nairobi. Hivyo basi tumeweza kubaini kuwa wanafunzi na wadau wengine katika shule za sekondari Nairobi, wana mielekeo chanya kuhusu lugha Sheng. Hata hivyo mielekeo hii huenda ikawa tofauti katika

miji mingine nchini Kenya. Hivyo basi, tafiti zingine zinafaa kufanywa kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusu Sheng katika miji mingine nchini Kenya ili kubaini mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine kuhusu Sheng ikizingatiwa kuwa miji mingine ina wazungumzaji wa lugha moja ya kwanza tofauti na mji wa Nairobi ambapo wanafunzi wanaosoma katika shule za sekondari hutoka maeneo yanayoishi watu wanaozungumza lugha tofauti za kwanza. Pia, utafiti huu umejikita katika shule ya upili, hivyo basi tafiti zaidi zinafaa kufanywa katika viwango vingine kama vile shule za msingi, vyuo vya ufundi, vyuo vya kati na hata katika vyuo vikuu nchini Kenya ili kubaini mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha ya Sheng katika viwango hivi. Vile vile utafiti huu umejikita katika shule ya wavulana na wala sio ya mseto au wasichana. Kwa hali hii, tunapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanywe kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari jijini Nairobi lakini kwa kuzingatia shule za mseto na zile za wasichana na pia kuangazia miktadha mingine kama vile ya sokoni na sehemu za burudani ambazo hatujaweza kuangazia kwa kuzingatia mipaka ambayo tumejipa katika utafiti huu. Matokeo ya tafiti kama hizi yatasaidia kubaini kinachoweza kufanywa ili kuzuia matokeo mabaya katika mitihani ya Kiswahili yanayoambatishwa na matumizi ya lugha ya Sheng. Isitoshe, nadharia ambayo tumetumia imetupa matokeo tuliyoyapata na kwa hiyo tunapendekeza kuwa nadharia zingine zitumike ili kuweza kuona kama matokeo yatakuwa yale yale au yatabadilika. Kwa kufanya hivyo, wapanga lugha na watoa sera za lugha nchini Kenya wataweza kufanya shughuli hii kwa kujiamini zaidi.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M. H. (1982) Patterns of Language Acquisition and Use in Kenya: Rural – Urban Differences. Katika Polome, E. (Mhr). *International Journal of the Sociology of Language*. Vol.34.
- Abdulaziz, M. H. na Osinde, K. (1997) 'Sheng' and Engsh. *Development of mixed codes among the urban youth in Kenya.* *International Journal of the Sociology of Language*. 125:43-65.
- Amanda, L. (2011) 'Pohamba's Namlish Offers Light Relief.' *The Namibian*. August 12.
- Baker, C. (1992) *Attitude to Language*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Buliba, A. Njogu, K. na Mwhaki, A. (2006) *Isimujamii kwa wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Cargile, A. C., Giles, H. (1997) *Understanding Language Attitudes: Exploring Affect and Identity*. *Language and Communication*. 17 (3), 195 – 217.
- Chacha L. M. na wengine, (2003). *AKS 100: Introduction to the study of Language: Kiswahili module*. Nairobi. Kenyatta University.
- Chambers, J. K. na Trudgil, P. (1980). *Dialectology*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi University Press
- Donald K. K. na Delno L.A. T. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Pauline's Publications Africa.
- Echessa, P. G. (1990) *A Study of the Word Structure and Processes involved in Word Formation In Sheng'*. A case study of Eastlands area in Nairobi. Unpublished Masters Thesis. UON.
- Fink, T. K. (2005) *Attitudes Towards Languages in Nairobi*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuucha Pittsburgh.
- Gardner R. C. na Lambert, W.E. (1959). *The Social-Psychological Theory of Second language (L2)*.
- Gardner, R.C. na Lambert, W.E. (1972) *Attitudes and Motivation in aSecond-Language Learning*. Massachusetts: Newbury House Publishers.
- Githinji, P. (2006) *Sheng and Variation. The Construction and Negotiation of Layered Identities*. Unpublished Phd dissertation. Michigan State University.

- Githinji, P. (2008) *Ambivalent Attitudes: Perception of Sheng' and its Speakers*. Ohio University: Nordic Journal of African Studies. 17(2), 113-136.
- Githiora, J. (2002) 'Sheng: *Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole?*' Journal of African Cultural Studies. University of London vol.15 pp159-183.
- Gorman, T. B. (1974) The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational System. Katika. W. H. (mhr). *Language in Kenya*. Nairobi: oxford University Press. 397 – 446.
- Habwe J. et. al (2010). *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyu*. Nairobi: Phoenix.
- Ipara I. O. na Maina G. (2008) *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Oxford University Press, EastAfrika Ltd.
- Iribe M. P.I. na Mukhwana A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi. Focus Publishers Ltd.
- Janet H. (2013) *An Introduction to Social Linguistics*. (4th edition) Routledge Taylor and Francis group London and New York.
- Jones, J. M. (2012) *The Effect of Language Attitudes on Kenyan Stakeholder Involvement in Mother tongue Policy Implementation*. Journal of Multilingual and Multicultural Development. 33 (3), 237 – 250.
- King'ei, K. (2010) *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI
- Kobia, J. (2006) 'Sheng is not a Language but a popular Slang.' Sunday Nation, Nairobi Feb. 2.
- Kachipela, D. (2014) *Athari za Sheng katika matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi mtaa wa Kangemi*. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado kuchapishwa. UON.
- Kachru B.B. (1977) *Code Switching as a Communicative Strategy of India in Saville - Troike, Murie (wah) Linguistic and Anthropology*. Washington Georgetown University.
- Kembo – Sure (2002) *Language Planning and National Development in Kenya*. Katika: Ingrid R. (mhr). Languages in Contact. Bayreuth: African Studies. Vol. 51.
- Kenyatta University School of Hospitality and Tourism. (2012). *Guidelines for writing Academic Research Proposals and Thesis Handbook*. Nairobi: Kenyatta University Printing Press.
- Kibiwott, P. K. (2006) *The Future of Language of Kenya: Adopting the Principles of Environmental Conservation*. Makala yaliyowasilishwa katika Kongamano la BAAL Linguistics in Africa Special Interest Group, Chuo Kikuu cha London.
- Kitsao J. (1975). "A stylistic Approach Adopted for the Study of Kiswahili Prose Texts". M.A. Thesis: Nairobi University. (Haijchapisha)

- Lambert, W.E. (1963b) Approaches to the Study of Language Part II: On the Second Language Learning and Bilingualism. *The Modern Language Journal*. 47(14), 114-121.
- Lambert, W.E., Hodson, R., Gardner, R.C. na Fillenbaum, S. (1960) Evaluational Reactions to Spoken Languages. *Journal of Abnormal and Social Psychology*. 60(1), 44-51.
- Larsen, M. H. (1992) *An Introduction to Language Two Acquisition Research*. Longman. London.
- Mathoko P.M. (2007) *Isimujamii; Misingi na Nadharia*. Njigua Books. Nairobi.
- Mazrui, A. M. (1978) The Religious Factor in Language Nationalism: The Case of Kiswahili in Kenya. *Katika: Studies in African Linguistics*. Vol.9. No. 21978. University of California.
- Mazrui, A. M. (1995) 'Slang and Code Switching: The Case of Sheng in Kenya.' *Africanistich arbeitspapier* 42:16 -179.
- Mbaabu, I. (1991) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mbaabu, I. (2003) *Sheng-English Dictionary*. University of Dar es Salaam. TUKI.
- Mbaabu, I. na Nzungu, K. (2003) *English-Kiswahili Dictionary of Sheng. Deciphering East Africa Underworld Language*. University of Dar es Salaam. TUKI.
- Mdee J.S. (1986). *Kiswahili: Muundo na Matumizi Yake*. Nairobi. Intercontinental Publishers Ltd.
- Mekacha, R.D.K. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Mukadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mkangi, K. (1984) 'Sheng and the Kenyan culture.' *The standard*. August. 30.
- Moga, J. na Fee, D. (1997). *Sheng Dictionary*. Nairobi. Ginsen Publishers.
- Mohochi, S. (2011) Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum*. 18: 24-36.
- Momanyi, C. (2009) 'Effects of Sheng in Teaching of Kiswahili in Kenyan schools'. *Journal of Pan African studies*. 12:127-128.
- Mpande, M. (1990) 'Sheng and the Kenyan culture.' *The standard*. August. 30.
- Msanjila, Y.P. et al (2009). *Isimujamii : Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G. (1999) *Research methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Africa centre for Technology studies. Nairobi.
- Mugenda, O.M. and Mugenda, A.G. (1990). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi. Acts Press.

- Mukhebi, I. (1986) *'Is Language and Culture Inseparable?'* Kenya Times, Nairobi, May 28.
- Mukhwana, A. (2008), *"Language Attitudes in Urban Kenya: A Case Study of Nairobi, Mombasa and Kisumu"*, Ph.D Thesis, Nairobi: University of Nairobi.
- Mukhwana, A. na Jerono, P. (2014) Language Attitudes in Colonial Kenya: An Historical Perspective. *International Journal of Education and Research*. Vol.2 No.3.
- Mweri, J. G. (2010) *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Myers - Scoton (1998). *Cote Switching as a Mechanism of deep borrowing; Language Shifting and Language death*. Brenzinger Mathias (mhr).
- Ndiku, L. Mwita, M. na Ocharo, G. (2014) *Students and Educator Perception of use of Sheng*. University of East Africa.
- Ngesa, M. (2012) *'And Sheng Lives on Profile.'* East Africa Standards 16-22 Feb.2012.
- Ngeumo, T.M (2008) *'The prevalence of Slang use among students of Basic Remedial Studies and its effect on the Teaching of English as a Second Language.'* Ahmadu Bello University.
- Njoroge, F. (2014) *Hali, hadhi na majukumu ya Sheng mjini Nakuru*. Tasnifu ya uzamilifu ambayo bado haijachapishwa.UON.
- Obuchi, M.S na Mukhwana, A. (2010) *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na vipengele*. Nairobi. Frame publishers.
- Odhiambo, G. (2013) *Athari za Sheng katika Dini ya Kikristo Mtaa wa Umoja*. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa. UON.
- Ogechi, N. O. (2004) *'On Lexicalization in Sheng.'* Nordic Journal of African Studies. Vol 2:325-342.
- Ogechi, N. O. (2005). *Does Sheng have a Kiswahili grammar?* AP.A.L Annual Publication in African Linguistics 3.3-25.
- Okoto, W. L. (2015). *Athari za Sheng kwa lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachapishwa.UON.
- Osinde, K. (1986) *Sheng: An investigation in to the Social and Structural Aspect of an Evolving Language*. Tasnifu ya B.A ambayo bado haijachapishwa. UON.
- Richards et al. (1985) *Longman Dictionary of Applied linguistics*.UK. Longman Group.
- Sabiti, B. (2015) *'One of the funniest and greatest English Varieties in the World.'* Daily Monitors, February 20.
- Shitemi, N.L. (2001) *'Pidginization: Sheng and Melting Pot of Kenyan Languages and Anti-babel Development.'* Dar es Salaam. Institute of Kiswahili Research.

- Syropoulos, M. (1987). 'Sheng some Preliminary Investigation into a Recently Emerged Nairobi Street Language.' *Journal of the Anthropological Society*. Oxford 18(2) 15-136.
- TUKI. (1990) *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu*. Dar es Salaam, University of Dar es Salaam.
- Waithira, C. (2011). *A Study of the Structure of Youth Jargons in Nairobi*. Unpublished phil. Thesis. Moi University.
- Warambo, P. (2011) *Uchanganuzi wa Maendeleo wa Kisemantiki katika Sheng: Mtazamo wa Pragmantiki Leksika*. Tasnifu ya uzamili ambayo bado haijachpishwa. UON.
- Wardhaugh, P. (1987). *Languages in Competition*. Oxford: Basic Blackwell co.
- Wardhaugh R. na Fuller M.J. (2015). *An Introduction to Sociolinguistics*. Wiley Blackwell Publishers Ltd.
- wa Thiong'o, N. (1986) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Webb na Kembo-Sure (1992) *Africa Voices; An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa*. Cape Town and New York. Oxford University Press.
- Whiteley, W. H. (1974) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Kutokana na utofauti wa wahojiwa na wale waliojaza hojaji, tulitayarisha hojaji nne tofauti ili kuweza kupata mitazamo ya wahusika tofauti tofauti. Hojaji zilizojazwa na wanafunzi, walimu, wazazi na wafanyikazi wengine wasio waalim na) hii ni sampuli tu ya maswali hayo ambayoyamegawanywa katika sehemu nne.

KIAMBATISHO 1

HOJAJI KWA WANAFUNZI

MASWALI KUHUSU MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WADAU WENGINE WA SHULE ZA SEKONDARI KUHUSU SHENG: KIFANI CHA SHULE YA UPILI YA JAMHURI, NAIROBI

Kwa majina naitwa Reuben Barasa. Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na ninafanya kozi ya shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng, huku nikirejelea shule ya upili ya Jamhuri. Tungependa kukueleza kuwa upo miongoni mwa wale walioteuliwa name ili kutupa habari ambayo naamini itakuwa ya manufaa katika uelewa juu ya mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng. Nakuhakikishia kuwa maelezo utakayonipa yatatumika kwa ajili ya utafiti huu pekee na kwamba yatahifadhiwa na kuwekwa siri. Unaombwa kwa heshima kujibu swali unaloulizwa kwa kutia mkwaju au kujaza jibu mwafaka katika sehemu zilizoachwa wazi.

Maswali

1. Umri wako?

2. Kidato chako?

Kidato cha kwanza

Kidato cha pili

Kidato cha tatu

Kidato cha nne

3. a) Je, ni miaka mingapi umekuwa shuleni hapa?
4. a) Je, makazi yako ni wapi hapa jijini?
5. a) Je, ni lugha gani unazozifahamu? Zitaje kwa usanjari unavyozitumia ukitanguliza ile uitumiayo zaidi.

6. Je, lugha iliyokuzaa na kukulea ni ipi? Na wewe huitumia katika mawasiliano ama la na kwa nini?

7. a) Je, Sheng ni lugha? Na wewe huitumia katika masiliano?

Ndio La

b) Ikiwa jawabu ni ndio, wewe huitumia wakati gani, na nani, kwa ajili gani na wapi?

.....

.....

.....

8. a) Je, wewe hutumia lugha ya Sheng ukiwa shuleni?

Ndio La

b) Toa maoni yako kulingana na jibu ulilotoa hapo juu.

.....

.....

.....

9. a) Je, unapendelea lugha ya Sheng au lugha ya Kiswahili sanifuna kwa nini?

Ndio La

b) Eleza zaidi kuhusu kauli uliyotoa hapo juu

.....
.....
.....

10. a) Je, unafikiri mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu?

Ndio

La

b) Fafanua kauli yako.

.....
.....
.....
.....

11. a) Je, matumizi ya lugha ya Sheng katika mawasiliano huathiri matokeo yako katika mtihani wa Kiswahili?

Ndio

La

b) Fafanua kauli yako.

.....
.....
.....
.....

12. a) Je, ni jinsia ya kiume ndio inayoyopendelea sana kutumia lugha ya Sheng ukilinganishwa na jinsia ya kike ama vinginevyo?

Kike

Kiume

Jinsia zote mbili

b) Toa maelezo yako kuhusiana na jibu ulilolitoa hapo juu?

.....
.....
.....
.....

13. a) Je, kuna uwezekano wa kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumiwa?

Ndio

La

b) Eleza sababu yako ya kusema hivyo

.....
.....
.....

14. Ni sababu gani zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu lugha moja, hasa lugha ya Sheng? Fafanua.

a)

.....

b)

.....

c)

.....

d)

.....

15. a) Je, kwa maoni yako mielekeo ya wazungumzaji inaweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....
.....

16. a) Je, matumizi ya lugha ya Sheng yameweza kuathiri utendakazi wako katika masomo mengine?

Ndio

La

b) Toa sababu zako kutokana na jibu lako la hapo juu.

.....
.....
.....

17. a) Je, mazingira unamoishi mnachangia katika mwelekeo wako kuhusiana na lugha ya Sheng?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....

18. a) Je, unadhani kuwa mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mwalimu au mzazi pamoja na wadau wengine wa shule hii?

Ndio

La

b) Toa ufafanuzi wa jibu lako.

.....
.....

19. Katiba mpya ya Kenya (2010) inampa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea. Nini, kwa maoni yako, mstakabali wa Sheng ikizingatiwa nafasi hii muhimu ambayo lugha na utamaduni vimepewa katika katiba hii?

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KWAKO KUJAZA HOJAJI HII.

KIAMBATISHO 2

HOJAJI KWA WALIMU

MASWALI KUHUSU MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WADAU WENGINE WA SHULE ZA SEKONDARI KUHUSU SHENG: KIFANI CHA SHULE YA UPILI YA JAMHURI, NAIROBI

Kwa majina naitwa Reuben Barasa. Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na ninafanya kozi ya shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng, huku nikirejelea shule ya upili ya Jamhuri. Tungependa kukueleza kuwa upo miongoni mwa wale walioteuliwa nami ili kunipa habari ambayo naamini itakuwa ya manufaa katika uelewa wangu juu ya mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng. Ninakuhakikishia kuwa maelezo utakayonipa yatumika kwa ajili ya utafiti huu pekee na kwamba yatahifadhiwa na kuwekwa siri. Unaombwa kwa heshima kujibu swali unaloulizwa kwa kutia mkwaju au kujaza jibu mwafaka katika sehemu zilizoachwa wazi.

Maswali

1. Jinsia yako?

Kike

Kiume

2. Umri wako?

3. Kiwango cha elimu?

Shule ya msingi

Shule ya upili

Chuo cha ufundi

Chuo Kikuu

4. a) Je, ni miaka mingapi umekuwa shuleni hapa?

5. a) Je, makazi yako ni wapi jijini Nairobi?

6. a) Je, ni lugha gani unazozifahamu? Zitaje kwa usanjari kutegemea ujuzi wako kuanzia ule wa juu zaidi.

7. Je, lugha iliyokuzaa na kukulea ni ipi? Na wewe huitumia katika mawasiliano ama la na kwa nini?

8. a) Je, Sheng ni lugha? Na wewe huitumia katika masiliano?

Ndio

La

b) Ikiwa jawabu ni ndio, wewe huitumia wakati gani, na nani, kwa ajili gani na wapi?

.....
.....
.....
.....

9. a) Je, wewe huitumia lugha ya Sheng ukiwa shuleni?

Ndio

La

b) Toa maoni yako kulingana na jibu ulilotoa hapo juu.

.....
.....
.....
.....

10. a) Je, unapendelea lugha ya Sheng au lugha ya Kiswahili sanifu?

Ndio

La

b) Elezazaidi kuhusu kauli uliyotoa.

.....
.....
.....
.....

11. a) Je, unafikiri mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu?

Ndio

La

b) Fafanua kauli yako.

.....
.....
.....
.....

12. a) Je, ni jinsia ya kiume ndio inayoyopendelea sana kutumia lugha ya Sheng ukilinganishwa na jinsia ya kike ama vinginevyo?

Kike

Kiume jinsia zote mbili

b) Toa maelezo kiufafanuzi kuhusiana na jibu ulilolitoa hapo juu?

.....
.....
.....
.....

13. a) Je, kuna uwezekano wa kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumiwa?

Ndio

La

b) Eleza sababu yako ya kusema hivyo

.....
.....
.....

14. Ni sababu gani zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu lugha moja, hasa lugha ya Sheng? Fafanua.

- a)
- b)
- c)
- d)

15. a) Je, kwa maoni yako, mielekeo ya wazungumzaji inaweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji?

Ndio La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....
.....

16. a) Je, matumizi haya ya lugha ya Sheng yameweza kuathiri matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili?

Ndio La

b) Toa sababu zako kutokana na jibu lako hapo juu.

.....
.....
.....

17. a) Je, mazingira anamoishi mzungumzaji huchangia katika mwelekeo wake kuhusiana na lugha ya Sheng?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....

18. a) Je, unadhani kuwa mielekeo kuhusu lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mwalimu au mzazi pamoja na wadau wengine wa shule hii?

Ndio

La

b) Toa ufafanuzi wa jibu lako.

.....
.....

19. Katiba mpya ya Kenya (2010) inampa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea. Nini, kwa maoni yako, mstakabali wa Sheng ikizingatiwa nafasi hii muhimu ambayo lugha na utamaduni vimepewa katika katiba hii?

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

..

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KWAKO KUJAZA HOJAJI HII.

KIAMBATISHO 3

HOJAJI KWA WAFANYIKAZI WASIO WALIMU

MASWALI KUHUSU MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WADAU WENGINE WA SHULE ZA SEKONDARI KUHUSU SHENG: KIFANI CHA SHULE YA UPILI YA JAMHURI, NAIROBI

Kwa majina naitwa Reuben Barasa. Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na ninafanya kozi ya shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng, huku nikirejelea shule ya upili ya Jamhuri. Ningependa kukueleza kuwa upo miongoni mwa wale walioteuliwa name ili kunipa habari ambayo naamini itakuwa ya manufaa katika uelewa juu ya mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng. Ninakuhakikishia kuwa maelezo utakayonipa yatatumika kwa ajili ya utafiti huu pekee na kwamba yatahifadhiwa na kuwekwa siri. Unaombwa kwa heshima kujibu swali unaloulizwa kwa kutia mkwaju au kujaza jibu mwafaka katika sehemu zilizoachwa wazi.

Maswali

1. Jinsia yako?

Kike

Kiume

2. Umri wako?

3. Kiwango cha elimu?

Shule ya msingi

Shule ya upili

Chuo cha ufundi

Chuo Kikuu

4. a) Je, ni miaka mingapi umekuwa shuleni hapa?
5. a) Je, makazi yako ni wapi jijini Nairobi?
6. a) Je, ni lugha gani unazozifahamu? Zitaje kwa usanjari huku ukitanguliza unavyozipendelea.
7. Je, lugha iliyokuzaa na kukulea ni ipi? Na wewe huitumia katika mawasiliano ama la na kwa nini?

8. a) Je, Sheng ni lugha? Na wewe huitumia katika masiliano?

Ndio La

- b) Ikiwa jawabu **nindio**, wewe huitumia wakati gani, na nani, kwa ajili gani na wapi?

.....

9. a) Je, wewe hutumia lugha ya Sheng ukiwa shuleni?

Ndio La

- b) Toa maoni yako kulingana na jibu ulilotoa hapo juu.

.....

10. a) Je, unapendelea lugha ya Sheng au lugha ya Kiswahili sanifu?

Sheng Kiswahili

b) Eleza kauli uliyotoana taja lugha nyingine iwapo sio Sheng wala Kiswahili

.....
.....
.....
.....

11. a) Je, unafikiri mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu?

Ndio

La

b) Fafanua kauli yako.

.....
.....
.....
.....

12. a) Je, ni jinsia ya kiume ndio inayoyopendelea sana kutumia lugha ya Sheng ukilinganishwa na jinsia ya kike ama vinginevyo?

Kike

Kiume

Jin zote mbili

b) Toa maelezo yako kuhusiana na jibu ulilolitoa hapo juu?

.....
.....
.....
.....

13. a) Je, kuna uwezekano wa kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumiwa?

Ndio

La

b) Eleza sababu yako

.....
.....
.....

14. Ni sababu gani zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu lugha moja, hasa lugha ya Sheng? Fafanua.

a.
.....

b.
.....

c.
.....

d.
.....

e. a) Je, kwa maoni yako, mielekeo ya wazungumzaji inaweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....
.....

f. a) Je, matumizi haya ya lugha ya Sheng yameweza kukupa uhusiano mwema na wanafunzi wanaozungumza lugha hii ya Sheng?

Ndio

La

b) Toa sababu zako kutokana na jibu lako hapo juu.

.....
.....
.....

g. a) Je, mazingira unamoishi yanachangia katika mwelekeo wako kuhusiana na lugha ya Sheng?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....

h. a) Je, unadhani kuwa mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mwalimu au mzazi pamoja na wadau wengine wa shule hii?

Ndio

La

b) Toa ufafanuzi wa jibu lako.

.....
.....

i. Katiba mpya ya Kenya (2010) inampa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea. Nini, kwa maoni yako, mstakabali wa Sheng ikizingatiwa nafasi hii muhimu ambayo lugha na utamaduni vimepewa katika katiba hii?

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

..

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KWAKO KUJAZA HOJAJI HII.

KIAMBATISHO 4

HOJAJI KWA WAZAZI

MASWALI KUHUSU MIELEKEO YA WANAFUNZI NA WADAU WENGINE WA SHULE ZA SEKONDARI KUHUSU SHENG: KIFANI CHA SHULE YA UPILI YA JAMHURI, NAIROBI

Kwa majina naitwa Reuben Barasa. Mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi na ninafanya kozi ya shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng, huku nikirejelea shule ya upili ya Jamhuri. Ningependa kukueleza kuwa upo miongoni mwa wale nami ili kunipa habari ambayo naamini itakuwa ya manufaa katika uelewa juu ya mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari Nairobi kuhusu Sheng. Ninakuhakikishia kuwa maelezo utakayonipa yatatumika kwa ajili ya utafiti huu pekee na kwamba yatahifadhiwa na kuwekwa siri. Unaombwa kwa heshima kujibu swali utakaloulizwa kwa kutia mkwaju au kujaza jibu mwafaka katika vijisehemu vilivyoachwa wazi.

Maswali

1. Jinsia yako?

Kike

Kiume

2. Umri wako?

3. Kiwango cha elimu?

Shule ya msingi

Shule ya upili

Chuo cha ufundi

Chuo Kikuu

4. a) Je, ni miaka mingapi umekuwa mzazi wa mwanafunzi shuleni hapa?
5. a) Je, makazi yako ni wapi jijini Nairobi?
6. a) Je, ni lugha gani unazozifahamu? Zitaje kwa usanjari kutegemea jinsi unavyozielewa.
7. Je, lugha iliyokuzaa na kukulea ni ipi? Na wewe huitumia katika mawasiliano ama la na kwa nini?

8. a) Je, Sheng ni lugha? Na wewe huitumia katika masiliano?

Ndio

La

- b) Ikiwa jawabu ni ndio, wewe huitumia wakati gani, na nani, kwa ajili gani na wapi?

.....

.....

.....

.....

9. a) Je, wewe hutumia lugha ya Sheng ukiwana mtoto wako au mwanafunzi yeyote wa shule hii?

Ndio

La

- b) Toa sababu yako kulingana na jibu ulilotoa hapo juu.

.....

.....

.....

.....

10. a) Je, unapendelea lugha ya Sheng?

Ndio

La

b) Toa sababu kauli uliyotoa

.....
.....
.....
.....

11. a) Je, unafikiri mielekeo ya watu wanaozungumza lugha ya Sheng huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu?

Ndio

La

b) Fafanua kauli yako.

.....
.....
.....
.....

12. a) Je, ni jinsia ya kiume ndio inayoyopendelea sana kutumia lugha ya Sheng ukilinganishwa na jinsia ya kike ama vinginevyo?

Kike

Kiume Jinsia zote mbili

b) Toa maelezo yako kuhusiana na jibu ulilolitoa hapo juu?

.....
.....
.....
.....

13. a) Je, kuna uwezekano wa kutoathiriwa na lugha ya Sheng hata iwapo unaishi katika mazingira ambamo lugha ya Sheng inatumiwa?

Ndio

La

b) Eleza sababu yako

.....
.....
.....

14. Ni sababu gani zinazoweza kumfanya mzungumzaji wa lugha fulani kuwa na mwelekeo chanya au hasi kuhusu lugha moja, hasa lugha ya Sheng? Fafanua.

- a.
.....
- b.
.....
- c.
.....
- d.
.....

15. a) Je, kwa maoni yako, mielekeo ya wazungumzaji inaweza kuathiri uteuzi na utumizi wa lugha fulani na mzungumzaji?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....
.....

16. a) Je, matumizi haya ya lugha ya Sheng yameweza kuathiri utendakazi wa mtoto wako na wanafunzi wengine unaowafahamu katika masomo yao mengine?

Ndio

La

b) Toa sababu zako kutokana na jibu lako hapo juu.

.....
.....
.....

17. a) Je, mazingira unayoishi yanachangia katika mwelekeo wako kuhusiana na lugha ya Sheng?

Ndio

La

b) Eleza sababu zako.

.....
.....

18. a) Je, unadhani kuwa mielekeo juu ya lugha ya Sheng inaweza kuathiri uhusiano baina ya mwanafunzi na mwalimu au mzazi pamoja na wadau wengine wa shule hii?

Ndio

La

b) Toa ufafanuzi wa jibu lako.

.....
.....

19. Katiba mpya ya Kenya (2010) inampa Mkenya uhuru wa kuchagua na kutumia lugha na utamaduni anaoupendelea. Nini, kwa maoni yako, mstakabali wa Sheng ikizingatiwa nafasi hii muhimu ambayo lugha na utamaduni vimepewa katika katiba hii?

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

..

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KWAKO KUJAZA HOJAJI HII.